Nipashe
Jumamosi Januari 11, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580125
www.ippmedia.com
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## ‘Hausi boi’ afungwa miaka 30 jela kumlawiti mtoto wa bosi

UKURASA 10




UKURASA 13

# Umeya wa Jiji Dar sasa kizungumkuti

**BAADA** ya akidi pungufu kumng’oa, korti yatupa pingamizi lake... *Endelea ukurasa wa 2*



Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Isaya Mwita (katikati), akitoka kusikiliza kesi ya kuvuliwa umeya katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana, ambapo mahakama hiyo, ilitupilia mbali maombi madogo ya kuomba zuio la meya huyo, kuondolewa kwenye nafasi yake. **PICHA: MIRAJI MSALA**



## SAMIA ASHUKIA VIJANA WA CCM

UKURASA 12




Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store


## Vigogo wawili Nida watumbuliwa

UKURASA 2

MICHEZO MBELGIJI WA YANGA KICHEKO, Z’BAR VILIO UK. 32
MAONI, KATUNI UK.6

# Umeya Dar sasa kaa la moto

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imetupilia mbali maombi madogo ya Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Isaya Mwita, kuweka zuio la kuondolewa kwenye nafasi yake.

Imeelezwa na mahakama hiyo kuwa sababu za kutupilia mbali maombi hayo ni kutowasilishwa uthibitisho wa kufanyika kikao cha kumwondoa madarakani wala hasara atakayoipata atakapoondolewa katika wadhifa huo.

Lakini, mahakama hiyo imekubali ombi la kwanza la kuongezwa muda wa kujibu hati kinzani ya walalamikiwa, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

Uamuzi huo ulisomwa jana na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Janeth Mtega, aliyesikiliza maombi hayo madogo.

Alisema kuwa baada ya kusikiliza hoja za mawakili wa pande zote mbili, mahakama imeona kwamba mlalamikaji ameshinda ombi lake la kwanza la kutaka kuongezwa muda wa kuwasilisha majibu ya hati kinzani.

Alisema ili mahakama isikilize kesi ya madai, ni lazima nyaraka zote muhimu zikamilike dhidi ya maombi ya msingi kwa mujibu wa sheria.

Kuhusu ombi la pili la mlalamikaji, mahakama imeona kwamba Wakili wake, Hakima Mwasipo, alikuwa na wajibu wa kuthibitisha uwapo wa kikao cha kumwondoa Mwita madarakani.

Alisema ni lazima mahakama ipewe maelezo juu ya uwapo wa kikao cha kumwondoa katika nafasi yake ya umeya ili ifikie uamuzi wa kutoa haki.

"Kwa kuwa mlalamikaji ameshindwa kuithibitishia mahakama hii kuhusu kikao cha kumwondoa kwenye nafasi yake ya umeya, inatupilia mbali hoja za kutaka abaki madarakani kwa sababu hoja zake kupitia wakili wake hazina miguu ya kusimamia kwa kushindwa kufuata vigezo ikiwamo kueleza kuhusu kufanyika kikao cha kutaka kumtoa madarakani," Hakimu Mtega alisema.

Alisema ili maombi yabaki katika nafasi yake, inatakiwa kuwapo kwa zuio la awali kuwezesha kitu hicho kubaki katika nafasi yake na kisiondoshwe.

Alisema mahakama hiyo ina maoni kwamba wakili wa mwombaji alikuwa na wajibu wa kuthibitisha uwapo wa kikao cha kumwondoa madarakani Mwita.

Akizungumzia hoja ya kesi kutajwa, Hakimu Mtega alisema kesi hiyo ilikuja Januari 8, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa na si kusikilizwa kwa kuwa bado mawakili walikuwa katika hatua ya kubadilishana nyaraka.

Alisema wakili wa wajibu maombi ambaye ni Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Gabriel Malata, alipotoka kwa kutaka mahakama iendelee na usikilizwaji wakati kesi hiyo imekuja kwa kutajwa.

Alisisitiza kuwa ni lazima mahakama ihakiki taratibu zote za usikilizaji wa shauri zinafuatwa kwa mawakili kubadilishana nyaraka ambazo ni hati ya kiapo, hati ya kiapo kinzani na majibu ya hati ya kiapo kinzani ndipo kesi ianze kusikilizwa.

Hata hivyo, alisema maombi ya msingi yenye usajili namba 3/2020, yatasikilizwa Januari 13, mwaka huu.

Katika madai ya msingi, Mwita anapinga mchakato wa kuondolewa kwenye nafasi yake ya umeya, akidai umekiuka utaratibu.

Meya huyo anadaiwa kupendelea madiwani wa chama chake katika uundaji wa kamati mbalimbali bila kumshirikisha Mkurugenzi wa Jiji, kutumia mali (gari) za ofisi vibaya na kushindwa kufanya matumizi ya hisa za Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA).

# Vigogo ununuzi waingia matatani

**Na Happiness Shayo, MKALAMA**

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa, amemwagiza Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Wilaya ya Mkalama, kuchunguza utendaji wa kitengo cha ununuzi cha wilaya hiyo kutokana na utekelezaji mbovu wa miradi ya maendeleo.

Agizo hilo alilitoa jana wakati wa kikao kazi na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama kilichofanyika kwenye ukumbi wa halmashauri hiyo.

"Nataka Takukuru mkichunguze kitengo cha ununuzi cha Wilaya ya Mkalama kwa sababu nimebaini kuna mwenendo mbaya katika utekelezaji wa miradi hapa wilayani," aliagiza. Mwanjelwa alidai kitengo hicho kimekuwa kikitoa zabuni za miradi mbalimbali bila kufuata utaratibu ikijumuisha pia upotevu wa vifaa vya ujenzi katika mazingira ya kutatanisha.

Alisema serikali imekuwa ikijitahidi kuhakikisha inafikisha huduma karibu na wananchi, akitolea mfano ujenzi wa hospitali, upanuzi wa vituo vya afya na ujenzi wa masoko, lakini wako baadhi ya watumishi wake wanaofanya ubadhirifu.

"Natoa onyo kwa watumishi ambao bado wanafikiria kujipatia fedha kupitia miradi hii na ninawapa pole kwa sababu serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dk. John Pombe Magufuli haitaki mzaha katika utendaji kazi," alitahadharisha.

Alisema serikali inataka watumishi walio safi kiutendaji, wanaowajibika ipasavyo na wanaofanya kazi kwa kufuata kanuni na taratibu za kiutumishi.

Katika hatua nyingine, Mwanjelwa amemwelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama kutekeleza agizo la serikali la kuwaondoa kazini watumishi wenye vyeti vya kughushi. Maelekezo hayo aliyatoa baada ya kupokea malalamiko ya Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Malela, Alfred Panda, aliyetaka kujua hatima ya mmoja wa walimu wake aliyebainika kuwa na cheti cha kughushi wakati wa kusafisha taarifa za watumishi, lakini amekuwa akiendelea na kazi na amefuatilia barua yake ya kusimamishwa kazi bila mafanikio.

Mwanjelwa alimtaka mkurugenzi huyo kulifanyia kazi suala la mtumishi huyo haraka iwezekanavyo. "Mkurugenzi hakikisha hatua kali za kisheria zinachukuliwa haraka kwa mtumishi huyu ambaye ana vyeti feki na unipe mrejesho," aliagiza. Naibu Waziri huyo yuko mkoani Singida kwa ziara ya kikazi yenye lengo la kukagua utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) na kukutana na watumishi ili kusikiliza kero zao na kuzitatua.



Mjumbe wa Kamati Kuu ya Taifa ya Halmashauri Kuu ya CCM na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akipokea Bendera ya Mapinduzi ya Zanzibar, kutoka kwa Daud Kalela mmoja kati ya vijana walioshiriki matembezi ya Vijana wa CCM kuelekea kilele cha Miaka 56 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar katika Uwanja wa Mapinduzi Square, Michenzani Zanzibar jana. **PICHA: OMR**

# Maofisa wawili Nida watumbuliwa

**Na Mwandishi Wetu,** SONGEA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amemwondoa madarakani Ofisa wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) Mkoa wa Ruvuma, Seif Mgonja, kwa madai ya kutogawa kwa wananchi namba za vitambulisho vya Taifa (NID).

Ofisa huyo anadaiwa kutogawa namba hizo kwa wananchi 14,493 tangu Desemba 31, mwaka jana licha ya kuzalishwa na makao makuu ya mamlaka hiyo na kupelekewa ofisini kwake mjini Songea.

Waziri Lugola pia amemwondoa madarakani Ofisa wa Nida Wilaya ya Namtumbo mkoani humo, Thobias Nangalaba, kwa madai ya uzembe kwa kutofika katika kikao chake na viongozi wa mkoa na wilaya, licha ya kupewa taarifa ya kuhudhuria kikao hicho.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara uliofanyika Viwanja vya Soko Kuu la Manispaa ya Songea jana, Waziri Lugola, alisema, ametengua vyeo vya maofisa wawili hao akidai wamecheza na kazi za serikali, kwa kutojali majukumu yao.

"Ndugu wananchi wa Songea, maofisa hawa wamekuwa wakienda kinyume cha maagizo ya serikali ya kuwataka wawakamilishie wananchi usajili wa laini za simu kwa alama za vidole kwa wakati.

Hivyo, hawatufai na wanapaswa watupishe ili wengine waweze kuiongoza Nida mkoani hapa. Haiwezekani ofisa wa Nida mkoa anacheza na

INAENDELEA UK. 8



Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James, akizungumza wakati wa uzinduzi wa mfumo wa serikali wa kielektroniki wa ukusanyaji mapato (GePG) uliofanyika jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Tahadhari mvua kubwa mikoa 7

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imetoa tahadhari ya kuwapo kwa siku mbili za mvua kubwa kwenye mikoa saba kuanzia jana.

Mikoa itakayopata mvua hiyo kwa mujibu wa TMA ni Singida, Rukwa, Mbeya, Iringa, Njombe, Songwe na Dodoma.

Meneja wa Utabiri kutoka Kituo Kikuu cha Utabiri TMA, Samuel Mbuya, aliwataka wakazi wa mikoa hiyo kuchukua tahadhari.

"Ni vyema watu wakachukua tahadhari ikiwamo kuzibua mifereji ili kuruhusu maji yasituame sehemu moja, maana hiyo ndiyo chanzo cha mafuriko, lakini pia kuhakikisha wanawahi kwenda kwenye maeneo yao ya kazi na kuondoa msongamano barabarani," alishauri.

Kwa mujibu wa meneja huyo, mamlaka itaendelea kutoa tahadhari, angalizo na taarifa mbalimbali za hali ya hewa kwa wananchi, ili kuwakinga na majanga yanayoweza kutokea kwenye jamii.

# NEC yakamilisha uandikishaji mikoa 25

**Na Elizabeth Zaya**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imekamilisha uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura katika mikoa 25 yenye halmashauri za wilaya 146 na majimbo 205 Tanzania Bara na Zanzibar.

Kwa mujibu wa NEC, mikoa ya Tanzania Bara amabyo kazi hiyo imefanyika ni pamoja na Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Simiyu, Mara, Mwanza, Kigoma, Tabora, Songwe, Kagera, Geita, Shinyanga, Katavi, Rukwa na Singida.

Mingine ni Dodoma, Mbeya, Iringa, Njombe na Ruvuma huku Zanzibar ikiboresha katika mikoa ya mikoa ya Kaskazini Pemba, Kusini Pemba, Kaskazini Unguja, Kusini Unguja na Mjini Magharibi.

Kwa mujibu wa taarifa ya NEC kwa vyombo vya habari jana, tume kwa sasa inajiandaa kuanza uboreshaji wa daftari katika mikoa ya Lindi na Mtwara na kwamba tayari mikutano ya wadau wakuu wa uchaguzi imefanyika.

Katika taarifa hiyo, NEC pia ilieleza kuwa elimu na hamasa kwa wananchi inaendelea kutolewa katika mikoa hiyo na kazi hiyo inatarajiwa kufanyika kwa siku saba kuanzia Januari 12 hadi 17.

NEC ilieleza katika taarifa yake hiyo kuwa awamu zilizobaki katika ukamilishaji wa kazi ya uboreshaji wa daftari hilo zinajumuisha mikoa ya Tanga na Morogoro katika Halmashauri za Miji ya Ifakara, Wilaya ya Malinyi na kazi itafanyika kuanzia Januari 23 hadi 29.

Tume hiyo ilisema itaendelea na uboreshaji wa daftari hilo katika wilaya za Gairo, KIlombero, Kilosa, Morogoro na Mvomero hadi Februari 9 mwaka huu.

Kwa mikoa ya Pwani na Dar es Salaam, uboreshaji umepangwa kufanyika kuanzia Februari 10 hadi 16.

NEC ilisema mchakato wa uboreshaji wa daftari hilo utahitimishwa kwa uwekaji wa wazi daftari hilo ili kutoa fursa kwa wananchi kuhakiki taarifa zao.

"Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa mujibu wa ibara ya 74 (6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ina jukumu la kuandikisha wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa Rais, wabunge na madiwani.

"Hivi sasa tume iko katika utekelezaji wa uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura ikiwa ni maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Uboreshaji huu unawahusu raia wa Tanzania ambao wametimiza miaka 18 na wale ambao watatimiza umri huo siku ya uchaguzi Oktoba."

"Pia unawahusu wale ambao wamehama kutoka maeneo yao ya awali kwenda maeneo mengine ya uchaguzi na wale ambao kadi zao zimeharibika au kupotea pamoja na kuwaondoa wale ambao wamepoteza sifa ya kuwapo katika daftari hilo hususani waliofariki dunia," NEC ilifafanua zaidi katika taarifa yake hiyo.

**"Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa mujibu wa ibara ya 74 (6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ina jukumu la kuandikisha wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa Rais, wabunge na madiwani.**


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **ADILI AUCTION MART COMPANY LIMITED & WAUNGWANA AUCTION MART, JAGRO AUCTION MART, KIBOKO AUCTIOON MART and JOSINA AUCTION MART** kwa niaba ya AccessBank Tanzania Limited watauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba, Magari na Viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kuwa utakapopita muda wa siku kumi na nne tangu kutoka kwa gazeti hili,dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada . Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| S/N | TAWI HUSIKA | KAMPUNI INAYO HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | KIJITONYAMA | ADILI AUCTION MART | MASOUD/YASSIN,AMIRI | MASOUD/YASSIN,AMIRI | NYUMBA YENYE BARUA YA MAUZIANO | MSAKUZI | 13/02/2020 SAA 11:00 ASUBUHI |
| 2 | KIJITONYAMA | WAUNGWANA | ABEL/ELITO, MILKA | ABEL/ELITO,MILKA | NYUMBA YENYE BARUA YA MAUZIANO | WAZO | 25/01/2020 SAA 11:00 ASUBUHI |
| 3 | KIJITONYAMA | WAUNGWANA AUCTION MART | KISEGA/IGNAS, FESTO | KISEGA/IGNAS,FESTO | NYUMBA YENYE BARUA YA MAUZIANO | MBAGALA | 22/01/2020 SAA 11:00 ASUBUHI |
| 4 | KIJITONYAMA | ADILI AUCTION MART | MWANGA/ROBERT,HOSANNA | MWANGA/ROBERT,HOSANNA | NYUMBA YENYE BARUA YA MAUZIANO | MISUGUSUGU | 21/02/2020 SAA 11:00 ASUBUHI |
| 5 | KIJITONYAMA | ADILI AUCTION MART | PALLANGYO/ MUINEI, ELIDAIMA | PALLANGYO/MUINEI, ELIDAIMA | KIWANJA | GOBA | 14/02/2020 SAA 11:00 ASUBUHI |
| 6 | KIJITONYAMA | ADILI SUCTION MART | SWAI/E,ROGATHE | SWAI/E,ROGATHE SAI/E,ROGATHE | NYUMBA YENYE BARUA YA MAUZIANO | MPIJI MAGOE | 17/02/2010 SAA 11:00 ASUBUHI |
| 7 | KIJITONYAMA | ADILI AUCTION MART | LYIMO/NICHOLAUS,AMANI | LYIMO/NICHOLAUS, AMANI | KIWANJA | GOBA | 28/01/2020 SAA 11:00 ASUBUHI |
| 8 | KIJITONYAMA | ADILI AUCTION MART | MARANDU/F, ERASMI | MARANDU/F,ERASMI | NYUMBA YENYE BARUA YA MAUZIANO | KIBWEGERE | 07/02/2020 SAA 11:00 ASUBUHI |
| 9 | PAMBA | JOSINA AUCTION MART | LWABUKOBA/ JOSEPH, BERNADO | LWABUKOBA/JOSEPH, BERNADO | TOYOTA RAV 4 T 142 CYU | NYASAKA CENTRE | 18/01/2020 ASUBUHI |
| 10 | PAMBA | KIBOKO AUCTION MART | BUJIGWA/K, JASTINE | BUJIGWA/K,JASTINE | NYUMBA | IGOMBE | 25/01/2020 ASUBUHI |
| 11 | PAMBA | KIBOKO AUCTION MART | ALLY/S,JASTINI | ALLY/S,JASTINI | NYUMBA | IGOMBE | 25/01/2020 ASUBUHI |
| 12 | PAMBA | JOSINA AUCTION MART | GILIGWA/I, GERARD | GILIGWA/I,GERARD | NYUMBA | KILIMAHEWA KWA MSUKA | 25/01/2020 ASUBUHI |
| 13 | MBEYA | JAGRO AUCTION MART | MWABULAMBO/E,CHRISTOPHER | MWABULAMBO/E,CHRISTOPHER | CAR NISSAN CALVAN T835CRD | UHINDINI | 27/01/2020 SAA 09:00 ASUBUHI |
| 14 | PAMBA | BOSTON AUCTION MART | LYAMBA/EMMANUEL, ENOCK | LYAMBA/EMMANUEL, ENOCK | MERCEDES BENZ T265DCH | NYASAKA CENTRE | 18/01/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**

1. UKAGUZI UNARUHUSIWA MARA USOMAPO TANGAZO HILI.
2. MNUNUZI ATALAZIMIKA KULIPA MALIPO YA 25% YA FEDHA TASLIMU PAPO HAPO NA 75% BAADA YA SIKU 14 TOKA SIKU YA MNADA KUFANYIKA NA UKISHINDWA KULIPA MALIPO YALIYOBAKI MNADA UTARUDIWA NA FEDHA ULIZO LIPA HAZITARUDISHWA
3. GHARAMA ZA KUBADILISHA UMILIKI NI ZA MNUNUZI MWENYEWE, KUMBUKA VIGEZO NA MASHARTI KUZINGATIWA.

KWA MAWASILIANO ZAIDI
0753077885 ADILI AUCTION MART
0713077474-WAUNGWANA AUCTION MMART
WOTE MNAKARIBISHWA.

215581302

# Katibu Mkuu aonya malipo ya serikali kufanyika kijima

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeziagiza taasisi za umma kuhakikisha zinatumia mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji mapato ya serikali (GePG), ili kuleta tija katika ukusanyaji wa mapato.

Rai hiyo ilitolewa jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James, wakati akifunga mkutano baina ya Wizara ya Fedha na idara, wakala wa taasisi na mashirika ya umma yaliyoko Kanda ya Kati, ambayo yameunganishwa na mfumo wa GePG.

Alisema licha ya jitihada kubwa zinazofanywa na Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha mfumo wa GEeG unaleta tija katika ukusanyaji wa fedha za umma, bado baadhi ya taasisi za umma hazijaboresha mifumo yake katika kuandaa ankara.

Alisema taasisi zote za umma zinawajibika kuhakikisha zinaendana na azma hiyo kwa kuboresha mifumo ya kielektroniki inayoandaa ankara ili kuwarahisishia walipaji huduma za serikali kupata ankara zao kwa ufanisi na haraka.

Alisema kwa kufanya hivyo, serikali itakusanya fedha kwa wakati na kutoa huduma bora kwa umma.

"Ili kuhakikisha mfumo wako unafuata viwango stahiki katika kuandaa taarifa ya ankara, hakikisha unawasiliana na idara ya usimamizi wa mifumo ya kifedha," aliagiza.

James alisema taasisi zote za umma nchini zinapaswa kutekeleza matakwa ya waraka namba tano wa Hazina unaozitaka kuhakikisha zinapata ridhaa ya Wizara ya Fedha na Mipango na Wakala wa Serikali Mtandao (eGA) kabla ya kufanya ununuzi, uandaaji, usimikaji na utumiaji wa mfumo wowote wa kielektroniki wa usimamizi wa fedha za umma.



Kijana mchuuzi wa nazi, akitoa huduma ya kuikuna kwa bei ya 100/- baada ya kumuuzia mteja wake katika eneo la Jeti Lumo- Mwisho wa Lami, jijini Dar es Salaam jana. Alisema ubunifu huo wa kibiashara umemwezesha kuuza nazi zaidi ya 100 kwa siku. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Polisi waahidi ulinzi sherehe za Mapinduzi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

JESHI la Polisi limesema kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, limepanga na kuweka mikakati kuhakikisha kunakuwapo na ulinzi wa kutosha katika sikukuu ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime, alisema kwa kutambua umuhimu wa sherehe hiyo ambayo pia ni kumbukumbu ya mapinduzi hayo, Jeshi la Polisi limejipanga kuimarisha ulinzi.

"Jeshi la Polisi tumejipanga kuhakikisha sherehe zinasherehekewa kwa amani, utulivu na usalama wa hali ya juu kabisa," Misime aliahidi.

Alisema mikoa na vikosi vyote vimepewa maelekezo na wamejipanga vizuri kuhakikisha hali ya amani inatawala kipindi chote cha sherehe hizo.

Hata hiyo, aliwataka wananchi kuwa umoja, amani, utulivu, usalama na mshikamano mkubwa katika sherehe hizo.

Alitoa wito kwa wananchi na wadau wote kuwa pamoja na kwamba Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama wameimarisha ulinzi na kuwataka wanapoona tukio au jambo lolote lisilo la kawaida, kutoa taarifa haraka kwa viongozi wa polisi na vyombo vingine vya ulinzi na usalama.

"Kama inavyofahamika Januari 12, mwaka huu, siku ya Jumapili Watanzania kwa ujumla wanasherehekea sikukuu ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Tumeimarisha ulinzi maeneo yote," alitamba.

Alisema siku hiyo ni muhimu kwa taifa kwa kuwa inakumbusha historia ya nchi.

Wakati huo, Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, amempongeza Rais John Magufuli kwa kuliwezesha jeshi hilo kuimarisha miundombinu yake mbalimbali ikiwamo mradi wa ujenzi wa nyumba 400 za makazi ya askari zilizojengwa nchi nzima.

IGP Sirro alisema jana kuwa ujenzi huo tayari umekamilika na askari wameanza kutumia nyumba hizo.

# Jafo awashukia maofisa utumishi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amekemea tabia ya baadhi ya maofisa utumishi kuchelewesha taarifa za baadhi ya watumishi pindi wanapopanda madaraja.

Jafo aliyasema hayo jana mjini hapa wakati wa maadhimisho ya Miaka 50 ya Shirika la Elimu Kibaha.

Alisema suala la maofisa utumishi kuchelewesha kuandaa miongozo kwa watumishi waliojiendeleza ni shida ambayo iko katika maeneo mbalimbali.

"Miongozo ya watumishi haitengenezwi na wanasiasa, si mkuu wa mkoa, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wala Jafo, inatengenezwa na wataalamu wenyewe na wanaolalamika ni wataalamu.

"Maofisa Utumishi mnatuangusha kwa kushindwa kuandaa bajeti kwa watumishi wanaopanda madaraja. Adui wa wataalamu ni wataalamu wenyewe, hata kupanda madaraja ni wataalamu wenyewe," alisema.

Aidha, Waziri Jafo alimwanguza Kaimu Mkurugenzi wa Shirika la Elimu Kibaha, Robert Shilingi, kushughulikia changamoto zilizoelezwa na Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, kuhusu baadhi ya watumishi wa idara ya afya.

Pia alimtaka mkuu wa mkoa kuwasiliana na mamlaka zinazohusika kuhakikisha wanatengeneza ruti maalumu kufika katika Hospitali ya Rufani Tumbi kwa kuwa sasa wagonjwa na wanaokwenda wanalazimika kukodi bajaji, pikipiki na teksi kwa usafiri.

Kuhusu uchakavu wa miundombinu, Waziri Jafo alisema, Serikali imetumia kiasi cha Sh. bilioni 49.9 kwa ajili ya ukarabati wa shule kongwe ikiwamo Kibaha Sekondari.

Awali, Ndikilo alisema watumishi wa Hospitali ya Tumbi baadhi yao wamekuwa wakilalamikiwa kuwa na kauli ambazo si rafiki kwa wagonjwa.

"Tutoeni huduma bora kwa wananchi. Tunalalamikiwa kuwa na lugha chafu kwa wagonjwa. Tunalalamikiwa kama mkoa, tuliokengeuka tujirekebishe," alisisitiza Ndikilo.

HABARI KITAIFA



Wachuuzi wa mishikaki na ndizi choma, wakiiandaa kwa ajili ya wateja wao, kando ya barabara ya Mabibo, nje ya Soko la Urafiki maarufu Mahakama ya Ndizi, jijini Dar es Salaam jana, katika mazingira hatarishi kiafya kutokana na vumbi linalosababishwa na magari. **PICHA: JOHN BADI**

# Waziri aitaka NHC kutafakari bei ya nyumba

**Na Munir Shemweta,** MASASI

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameitaka Bodi ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kupitia upya gharama za nyumba zake ilizojenga maeneo ya pembezoni kwa ajili ya kuziuza.

Dk. Mabula alitoa kauli hiyo juzi wilayani hapa alipotembelea mradi wa nyumba 54 zilizojengwa na NHC akiwa katika ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi katika mikoa ya kusini na kutembelea miradi inayofanywa na NHC katika maeneo mbalimbali nchini.

Alitoa kauli hiyo kutokana na kulalamikiwa na wabunge wa Masasi, Rashid Chuachua, na wa Lulindi, Jerome Bwanausi, kuwa pamoja na halmashauri kuhitaji nyumba kwa ajili ya watumishi, gharama zimekuwa kubwa kiasi cha halmashauri na wananchi kushindwa kuzinunua.

"Ni vizuri bodi ikae iangalia namna ya kupitia upya gharama za nyumba zote zilizoko maeneo ya pembezoni kama hizi za Masasi maana zikiachwa bila kununuliwa, itakuwa hasara," alisema.

Dk. Mabula alisema hata kama nyumba hizo zilizojengwa kwa ajili ya kuuza hazitanunuliwa, NHC iangalie namna ya kuzipangisha na kueleza uhitaji wa nyumba katika eneo la Masasi upo na watumisi wa serikali wanahitaji kuishi maeneo rafiki.

Pia alizitaka halmashauri nchini kuitumia NHC kujenga miradi ya nyumba za watumishi kulingana na mahitaji ili kuepuka kujenga nyumba ambazo zinaweza zisinunuliwe. Meneja Mawasiliano wa NHC, Muungano Saguya, alisema shirika lake liko katika hatua za mwisho za kukamilisha mradi huo uliokuwa umesimama kwa muda na kwamba takriban Sh. milioni 600 zitatumika kuukamilisha na kusisitiza kuwa ni imani yake katika miezi sita ujenzi utakamilika.

Kwa mujibu wa Saguya, bei inayolalamikiwa ya Sh. milioni 54 kwa nyumba moja inatokana na gharama kubwa iliyotumiwa na shirika kuzijenga na kubainisha kuwa NHC iko mbioni kuzipangisha baadhi ya nyumba ambazo wananchi wameonyesha nia ya kupanga.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri Mabula alizitembelea wilaya za Nanyumbu na Tunduru na kukagua utendaji kazi katika sekta ya ardhi katika halmashauri za wilaya hizo.

Mabula kwenye ziara hizo, alibaini utunzaji mbovu wa kumbukumbu za majalada ya ardhi pamoja na kiasi kidogo cha makusanyo ya maduhuli ya serikali kupitia kodi ya pango.

Kutokana na kasi hiyo ndogo, aliziagiza halmashauri za Nanyumbu na Tunduru kuongeza kasi ya makusanyo ya kodi ya pango la ardhi sambamba na kuzingatia utunzaji majalada ya ardhi kwa kufuata taratibu ikiwamo kuwapo mawasiliano katika majalada hayo kutoka ofisi mmoja kwenda kwa mwingine.

# Mabasi mtegoni usafirishaji vipeto

**Na Mwandishi Wetu**

MABASI ya abiria yanayofanya safari za mikoani, yamepigwa marufuku kubeba vifurushi bila kuwa na leseni kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Onyo hilo lilitolewa juzi na Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye, alipokuwa akifungua Baraza la Wafanyakazi wa Shirika la Posta (TPC) jijini Dodoma.

Kutokana na kuwapo kwa mabasi hayo yanayobeba mizigo bila leseni, Nditiye aliiagiza TCRA kuanza msako mara moja kuyabaini yanayokiuka sheria hiyo na kuyachukulia hatua. Nditiye alisema kwa mujibu wa Sheria ya TCRA, hakuna chombo chochote cha usafiri kinachopruhusiwa kubeba vipeto bila kuwa na leseni kutoka mamlaka hiyo na yeyote atakayekwenda kuinyune atachukuliwa hatua za kisheria.

"Kwa muda mrefu baadhi ya mabasi ya kwenda mikoani yamekuwa yakisafirisha mizigo, barua, vipeto na hata vyeti mbalimbali nyeti bila kufuata sheria na taratibu. Sasa hii ni lazima ifike mwisho. "Kuanzia sasa nimeiagiza TCRA kuanza kufanya msako dhidi ya basi moja hadi lingine. Ni lazima sheria zinazohusu uchukuzi zifuatwe na kuheshimiwa na niwajulishe wananchi kwamba usafirishaji wa vipeto na hata barua unafanywa na kampuni zilizosajiliwa na kupewa leseni na mamlaka ya mawasiliano," alisema. Katika kutekeleza hilo, Naibu Waziri aliiagiza TCRA kufanya ukaguzi kwenye vituo wakati mabasi yanapoanza safari na kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria kama ambavyo Mamlaka ya Usafiri wa Ardhini (Latra) inavyofanya.

Usafirishaji wa vipeto na bahasha ndani na nje ya nchi hufanywa na kampuni zilizosajiliwa kisheria na kupewa leseni na mamlaka ya mawasiliano nchini.

Miongoni mwa kampuni hizo ni TPC kupitia kampuni yake tanzu ya Expedited Mail Services (EMS), CDS Couriers, DHL Global Forwarding, SkyNet Worldwide Express, Zip N Zap Courier, TNT Express, MSS Logistics and Courier na Aramex Tanzania Limited.

# Waishukuru serikali kwa kuwakumbuka

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

UONGOZI wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Masasi mkoani Mtwara (FDC), umeishukuru serikali kwa kuwapatia fedha Sh. milioni 570.1 kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya chuo na kujenga majengo mengine mapya sita.

Umesema chuo kilikuwa kinakabiliwa na tatizo la uchakavu wa majengo yake hasa mabweni ya wanafunzi na madarasa, hali iliyousukuma uongozi kuiomba fedha serikalini.

Mkuu wa chuo hicho, Alfani Mshana, alitoa shukrani hizo kwa serikali jana alipozungumza na Nipashe ofisini kwake kuhusu vikwazo vinavyokikabili chuo hicho.

Mshana alisema tayari wameshapokea fedha hizo zilizotolewa na serikali kwa ajili ya ukarabati wa majengo yote chakavu.

Alisema ukarabati wa majengo na ujenzi wa majengo mapya sita katika chuo hicho tayari umeshaanza na baadhi ya majengo ukarabati wake unatarajia kukamalika hivi karibuni.

"Tunamshukuru sana Rais John Magufuli kwa kutupatia fedha hizi Sh. milioni 570.1 ili tukarabati majengo ya chuo hiki na kujenga mengine mapya, likiwamo bweni la wanafunzi," alisifu.

Alibainisha kuwa chuo hicho kina wanafunzi wapatao 300 ambao ni wasichana na wavulana, hivyo uboreshaji huo unaofanywa na serikali, utasaidia kukipa hadhi.

Hata hivyo, Mchana aliweka wazi kuwa bado jamii hasa ya mikoa ya kusini haijawa na mwamko chanya wa kutambua thamani ya uwapo wa chuo hicho, akieleza kuwa hata hamasa ya kuwapeleka watoto wao kusoma hapo bado ni ndogo.

Alisema chuo hicho kinatoa elimu ya fani mbalimbali kwa wanafunzi, ikiwamo stadi za maisha, ushonaji, uashi, mapishi, utengenezaji wa magari na umeme wa majumbani na magari.

Mshana alisema kupitia fani hizo zinazotolewa chuoni hapo, tayari chuo hicho kimeshazalisha wanafunzi wengi nchini ambao kwa sasa wamejiajiri na baadhi wameajiriwa katika sekta za umma na binafsi.

"Licha ya serikali kutupatia fedha hizi kwa ajili ya vikwazo vilivyokuwapo vya uchakavu wa majengo, tatizo lingine ni upungufu wa walimu, tuna walimu saba wakati mahitaji ni zaidi ya hapo," alibainisha.

Mwalimu Maliki Liyanga wa chuo hicho, pia aliishukuru serikali kwa kutoa fedha za ukarabati na ujenzi wa majengo mapya chuoni hapo.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Mungu ibariki Tanzania kuelekea fainali za Dunia*

**KWA** mara nyingine, bendera ya Tanzania kupitia mchezo wa soka inatarajiwa kupeperushwa katika kampeni ya kuwania tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Dunia kwa wanawake wa umri chini ya miaka 17.

Fainali hizo zitakazosimamiwa na Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), zitafanyika baadaye mwaka huu huko nchini India.

Katika safari hiyo, kikosi cha Tanzania ambacho kiko chini ya Kocha Mkuu, Bakari Shime 'Mchawi Mweusi' kitaanza kampeni hiyo kesho kwenye Uwanja wa Taifa kwa kuwakaribisha wenzao kutoka Burundi, huku wakitarajiwa kurudiana baada ya wiki moja mjini Bujumbura.

Ili malengo ya nchi na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), yatimie, ni wakati wa mashabiki kutoka sehemu mbalimbali kujitokeza kwa wingi kuwashangilia vijana hawa ambao wanahitaji kuanza vizuri mashindano hayo, wakiwa kwenye uwanja wa nyumbani.

Kama tunavyoamini na kukubali kwamba shabiki ni mchezaji wa 12, tunatakiwa tujitokeze kwa wingi kwenda kuwashangilia mabinti hawa ambao hapo baadaye tunatarajia kuwaona kwenye kikosi cha wakubwa maarufu Twiga Stars.

Timu hii ikiwa nyumbani, tunatakiwa kuitendea haki kwa kufika uwanjani kuwashangilia na kudhihirisha wako kwenye ardhi ya nyumbani kwa kuwaunga mkono kuwashangilia katika muda wote wa mchezo.

Nipashe inawaomba wadau wa michezo yote walioko jijini Dar es Salaam na mikoa ya jirani kujitokeza kuwashangilia mabinti hawa ili wafanye vema kama walivyofanikiwa kupeperusha vizuri bendera ya nchi katika mashindano ya Kombe la Chalenji iliyofanyika kwa kushirikisha timu sita za Afrika Mashariki na Kati kwa kumaliza kwenye nafasi ya pili.

Hakuna timu ambayo inaweza kupata mafanikio kama haitakuwa karibu na mashabiki wake, ukaribu na mashabiki huwafanya wachezaji kujiona wana deni la kusaka matokeo chanya na hali hii huwaongezea ari katika kupambana kusaka ushindi.

Tunaamini kwa upande wa ufundi, shime na benchi lake limekamilisha programu zote muhimu kuelekea mchezo huu wa kwanza, huku ikiyafanyia kazi upungufu uliyojitokeza wakati timu hizo zilipokutana Jinja, Uganda na matokeo kuwa sare ya mabao 3-3.

Kutopoteza mchezo hata mmoja kwenye mechi sita ilizocheza huko Uganda, ni dalili nzuri kwamba wachezaji wa timu hii wameiva na wanatakiwa kuingia uwanjani kesho wakiwaheshimu wapinzani wao.

Ni makosa kuingia uwanjani ukiwa na matokeo mfukoni, tunawaombea vijana wetu washuke dimbani wakifahamu Watanzania wanahitaji kupata ushindi na hatimaye kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kusonga mbele, huku wakifahamu watakuwa na kibarua kizito endapo wataiondoa Burundi.

TFF pia kwa upande wao inatakiwa kukamilisha majukumu yote ya kiutawala na kinachosubiriwa ni mchezo.

Uamuzi wa TFF kutoweka kiingilio katika eneo la mzunguko ambalo ndilo linaingiza idadi kubwa ya mashabiki, halijafanywa kimakosa, uamuzi huu umelenga mashabiki na haswa wanawake kufika uwanjani kuwashangilia watoto wao ambao wanapeperusha bendera ya nchi.

Hakuna mafanikio ambayo yatapatikana bila ya uwekezaji sahihi, kufanya vizuri kwa timu hii, ni ishara nzuri kwa Tanzania kutawala kwenye soka la wanawake kwenye ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati.

Soka halihitaji miujiza, tunaamini mafunzo waliyopokea wachezaji wa timu hii na mechi za kirafiki walizocheza, yatatupatia matokeo chanya katika mechi ya kesho.

Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki kikosi cha vijana cha wanawake cha U-17.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Barnabas Maro

# Muungwana Lazima Nilonge

## *Maneno ya mwenda wazimu...*

**NAPENDA** sana methali tulizoachiwa na wahenga wetu. Kila nisomapo hutafakari sana jinsi walivyojaaliwa hekima na Mwenyezi Mungu. Yote waliyosema enzi zao ndio yatokeayo sasa.

'Shabiki' ni mtu mwenye mapenzi na hamasa kubwa ya jambo au kitu. Mfano ni mashabiki wa kandanda duniani kote ingawa hapa nawazungumzia mashabiki wa Simba na Yanga, kabla na baada ya mechi zinazowakutanisha.

Januari 4, 2020 Simba na Yanga zilipambana kwa mara ya kwanza katika msimu wa Ligi Kuu inayoendelea sasa.

Husemwa "Maneno ya mwenda wazimu hayana maana lakini ni maneno." Maana yake maneno asemayo kichaa hayana maana kwake lakini ni maneno.

Twakumbushwa kwamba inafaa kusikiliza maneno yasemwayo na watu wengine hata kama tunawadharau kwa kuwa huenda yakawa na busara fulani.

Kabla ya pambano la Simba na Yanga mashabiki wa pande zote mbili walikuwa na maneno mengi ya kejeli (maneno ya kuonyesha dharau) kwa timu pinzani.

Mashabiki wa Simba ndiwo waliokuwa na maneno mengi sana dhidi ya Yanga. Walikuwa na kila sababu ya kuwatambia wenzao kwa jinsi timu yao ilivyo na wachezaji mahiri.

Wachezaji wao wamekuwa pamoja kwa muda mrefu na kuifanya timu yao iongoze Ligi Kuu kwa mabao mengi ya kufunga na machache ya kufungwa. Simba ina alama nyingi zaidi ya timu zote 20 zinazoshiriki Ligi Kuu, ikiwamo Yanga.

Kwa upande wa Yanga, ni mashabiki wachache wenye mioyo isiyo na wasiwasi walioweza kupambana na wenzao wa Simba kujibu mapigo. Wakati Simba wakisema Yanga ingefungwa si chini ya mabao 6-0, Yanga walijibu wakisema himaya ya Simba itashushwa, na Yanga kutwaa nafasi hiyo!

Maneno ya Simba yaliwaogofya baadhi ya mashabiki wa Yanga na kuwafanya kutokwenda uwanjani kushuhudia jinsi timu yao itakavyopigwa mabao 6-0 na Simba! Haikushangaza kuona Simba wakiwa wengi zaidi uwanjani.

Kwa wafuatiliaji wa mapambano ya Simba na Yanga, wanajua kuwa mara nyingi timu dhaifu ndio huishinda timu iliyokamilika kiuchezaji. Hutokea mara nyingi hata kuwashangaza watazamaji wa pande zote mbili.

Baada ya kile kisichotegemewa kufanyika, ndipo maneno ya "ilikuwaje ...imekuwaje" husikika kwa mashabiki na wanachama wa timu hizo.

Wahenga walisema "Maneno makali hayavunji mfupa" wakiwa na maana kuwa maneno tu hayawezi kuvunja mifupa hata yakawa makali kiasi gani.

Kadhalika ilisemwa na wahenga kuwa "Maneno ni daraja, hayazuii maji kuteremka." Maana yake daraja haliwezi kuyazuia maji ya mto yasiteremke. Kadhalika maneno nayo hayawezi kumzuia mtu kufanya jambo aliloazimia.

Kipindi cha pili kilipoanza, Simba ilifunga bao la pili lililofanya mashabiki wa Simba washangilie kwa hoihoi za kila aina huku wenzao wa Yanga wakiduwaa wasijue kinachoendelea!

Yanga ilipata bao la kwanza na la pili kwa muda usiozidi dakika saba. Sasa ikawa zamu ya mashabiki wa Yanga kutamba kwa nderemo huku wenzao wa Simba wakipigwa na bumbuazi (hali ya kutulia kimya kwa muda bila ya kujua la kufanya; butaa, mzubao).

Kwa hakika ni tukio ambalo halikutegemewa na mashabiki wa Yanga. Kabla ya kurejesha mabao hayo, wapo waliokata tamaa na kuanza kuondoka lakini bao la kusawazisha na kuwa 2-2 liliwarejesha uwanjani kwa shangwe!

Je, wanachama na mashabiki wa pande zote mbili wanasahau mwaka Yanga ilipoifunga Simba mabao 3-0 kipindi cha kwanza, lakini Simba ikasawazisha kipindi cha pili na kufanya matokeo kuwa sare ya 3-3 mpaka mwisho wa mchezo? Wakati ule kocha wa Simba alikuwa Abdallah Kibadeni.

Huu ndio ubishi na tambo nilizokuta katika moja ya mitaa ya Kariakoo majuzi. Shabiki wa Yanga alikuwa akitamba kwa timu yake kurejesha mabao mawili ya Simba kwa muda mfupi kuliko yaliyofungwa na Simba kwa kila kipindi bao moja.

Shabiki wa Simba alibeza sare ya timu hizo kwa kuwatusi (sipati herufi za kuandika neno chafu alilosema shabiki huyo)Yanga akisema: "eti Yanga kusawazisha kwao ndio ushindi ..." kisha akatoa tusi zito kwa watu wa Jangwani wanaosherehekea sare!

Waingereza husema kandanda ni mchezo wa kubahatisha. Naam, timu yaweza kucheza vizuri sana kama walivyokuwa Simba, lakini ikashindwa na timu inayobezwa na watazamaji. Ndio mambo ya ushindani, hasa mchezo wa kandanda.

Mchezo wowote ni jambo ambalo watu au timu hufanya kwa kushindana ili kujifurahisha na kuwafurahisha watazamaji hasa timu moja inapopata ushindi. Hakuna sababu ya kuchukiana, kutukanana wala kupigana!

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

# DC awanyooshea kidole watendaji uchafu

**Na Happy Severine,**
BARIADI

MKUU wa Wilaya ya Bariadi, Festo Kiswaga, amewatwisha mzigo wa lawana Ofisa Afya na watendaji wake katika halmashauri yake kwa kile anachodai kushindwa kuwajibika kutokana na Mji wa Bariadi ambao ni makao makuu ya Mkoa wa Simiyu, kukithiri kwa uchafu.

Kiswaga pia amedai Katibu Tarafa ya Bariadi na watendaji wa kata hiyo, ndiyo sababu ya mji huo kukithiri kwa uchafu.

Mkuu wa Wilaya huyo alishusha lawama hizo jana katika kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo, kilichofanyika katika Ukumbi wa Bardeco mjini hapa.

Alisema wanaotakiwa kubeba mzigo wa lawama ni watendaji hao, ambao alidai wameshindwa kuwasimamia wananchi kuhakikisha mji unakuwa safi.

"Hatuwezi kuwa na mji ambao serikali imewekeza zaidi ya Sh. bilioni 20 halafu ni mchafu, Ofisa Afya na Usafi wa Mazingira na Katibu Tarafa lazima wajitafakari katika hili, kama hawawezi, kuna sehemu nyingine za kufanya kazi.

"Kila sehemu ni uchafu, mitaro yote michafu, imefikia hatua mimi mwenyewe naingia mtaani kusimamia wananchi wafanye usafi wakati wahusika wapo, sasa nitoe onyo, sitafanya kazi za watu ambao hawawezi kuwajibika," alitahadharisha.

Kiswaga aliwataka watumishi hao kwa kushirikiana na watendaji wa mitaa na kata kuhakikisha wanasimamia suala la afya, huku akionya wanasiasa, hasa madiwani, kuingilia usimamizi wa suala hilo.



Mkuu wa Shule ya St. Anne Marie Academy, Gladius Ndyetabura, akiwapa zawadi ya fedha wanafunzi tisa wa shule hiyo, walioingia 10 bora kitaifa kwenye matokeo ya darasa la nne katika hafla fupi iliyofanyika shuleni hapo, jijini Dar es Salaam jana. Shule hiyo imekuwa ya kwanza kwa Mkoa wa Dar es Salaam na Wilaya ya Ubungo kwenye matokeo hayo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Shule yaibuka tena kinara matokeo ya mitihani Dar

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE ya St. Anne Marie Academy imeshika nafasi ya kwanza kwa Mkoa wa Dar es Salaam katika matokeo ya darasa la nne, huku wanafunzi wake tisa wakiingia 10 bora kitaifa kwa wasichana na wavulana.

Kwenye matokeo hayo yaliyotangazwa na Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA), shule hiyo imefanikiwa pia kuwa ya kwanza kwa Wilaya ya Ubungo na kuwa ya tisa kitaifa.

Mkuu wa shule hiyo iliyoko Mbezi Kwa Msuguri, Gladius Ndyetabura, alisema kwenye matokeo hayo, wanafunzi wote waliofanya mtihani wa darasa la nne walipata wastani wa alama A.

"Hakuna hata mwanafunzi mmoja aliyepata darala B, C, D wala E na mbali na hilo wanafunzi wetu 10 wamefanikiwa kuingia 10 bora kitaifa tunashukuru sana walimu kwa mafanikio haya, maana kuwa na wanafunzi 130 na wote kupata daraja A na kuingiza tisa 10 bora si kazi rahisi," alisema.

Alisema wanafunzi wa shule hiyo walioingia 10 bora kwa wavulana ni Elisha Mphuru aliyeshika nafasi ya pili kitaifa, Juma Bufe nafasi ya tatu kitaifa na Abdalah Lipagila nafasi ya saba kitaifa.

Ndyetabura aliwataja wasichana wa shule hiyo walioingia 10 bora kuwa ni Bernice Mwakalinga ambaye ameshika nafasi ya sita kitaifa, Dorine Komba nafasi ya saba na Zanula Mpandula ambaye ameshika nafasi ya nane.

Kwa upande wa kidato cha nne, alisema wanafunzi 43 wamepata daraja la I, wanafunzi 63 daraja la II, wanafunzi 19 daraja la III na wanafunzi sita daraja la nne.

Kuhusu matokeo ya kidato cha pili, Ndyetabura alisema wanafunzi 49 walipata daraja la I, wanafunzi 22 daraja la II, wanafunzi 23 daraja la tatu na wanafunzi saba daraja la nne.

Alitaja siri ya mafanikio ya shule yake kuwa ni kufundisha kwa bidii na kufuatilia maendeleo ya kitaaluma ya wanafunzi wake na kwamba mwaka huu wanatarajia kufanya vizuri zaidi kwenye matokeo ya darasa la saba.

"Kusimamia nidhamu ya wanafunzi na kushirikiana na wazazi ni moja ya siri ya mafanikio ya shule hii na pongezi tulizopata ni motisha kwamba tunatarajia kufanya vizuri zaidi ya hapa," alisema.

Ndyetabura alisema kwenye matokeo ya darasa la saba mwaka 2018, St' Anne Marie ilikuwa ya kwanza kwa Wilaya ya Ubungo, ya kwanza kwa Mkoa wa Dar es Salaaam na ya sita kwenye ngazi ya kitaifa.

"Tumekuwa tukifanya vizuri mwaka hadi mwaka kwenye matokeo ya wilaya, mkoa na kitaifa na kutokana na maandalizi mazuri tuliyoyafanya kwa wanafunzi wetu mwaka huu tunatarajia kufanya vizuri sana kwenye matokeo ya darasa la saba," alisema.

Aliwashukuru wazazi wa wanafunzi kuwa wamekuwa chachu ya ushindi wa shule hiyo kutokana na ushirikiano wanaotoa kwa uongozi wa shule hiyo kuanzia shule ya msingi hadi sekondari.

Ndyetabura aliwashukuru pia walimu wa shule hiyo kwa namna wanavyojituma usiku na mchana kuhakikisha wanafunzi wanaofanya mtihani wanapata alama za juu.

"Shukrani za kipekee ziwaendee walimu wangu kwa sababu hawapumziki wanafanyakazi usiku na mchana, Mkurugenzi wa shule Jasson Rweikiza naye amekuwa nguzo kubwa kwenye ushindi huu kwa namna anavyotupa kila aina ya ushirikiano tunampongeza sana," alisema.

# Bodi ya Maji mtegoni mapato

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZIRI wa Maji, Profesa Makame Mbarawa, ameiagiza Bodi mpya ya Maji ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (Shuwasa), kuhakikisha inasimamia ukusanyaji wa mapato na yasipungue Sh. milioni 700 kila mwezi.

Profesa Mbarawa alitoa agizo hilo juzi mjini Shinyanga alipokuwa akivunja bodi ya zamani ya mamlaka hiyo iliyomaliza muda wake na kuzindua bodi mpya, akionya kuwa endapo wakishindwa kufanya hivyo, hatakuwa na subira kuivunja.

Alisema hataki ukusanyaji wa mapato legevu unaokwamisha jitihada za serikali katika kupanua mtandao wa maji na kufikia wakazi wote wa Shinyanga.

Alisema kipimo cha kwanza kwa bodi hiyo mpya ya maji ambayo inaongozwa na Mwenyekiti Mwamvua Jilumbi, ni kuhakikisha ukusanyaji wa mapato unaongezeka na kuwa si chini ya Sh. milioni 700 kila mwezi.

"Kazi ya kwanza ambayo natoa kwa bodi hii mpya ya maji (Shuwasa) ni kwamba nataka mkusanye mapato yasiyopungua Sh. milioni 700 kila mwezi, mkishindwa kukusanya sitakuwa na msalie mtume kuvunja bodi hii.

"Pesa mtakayokusanya muitumie kuilipa Mamlaka ya Usambazaji Maji kutoka Ziwa Victoria (Kashwasa), ili mpanue mtandao wa maji, siyo kila siku mje kuomba fedha wizarani, fedha mnayopata ipelekeni kwenye miradi, na mjenge miradi hiyo ninyi wenyewe kwa kutumia makandarasi wa ndani," aliagiza.

Waziri huyo pia aliitahadharisha bodi hiyo kutojaribu kutumia fedha za mapato kujilipa posho na kupeana safari zisizo na tija, na kubainisha kuwa Shuwasa siyo mahala pa kula fedha, bali ni kwa ajili ya kusaidia wananchi wapate majisafi na ya kutosha.

Mwenyekiti wa bodi hiyo mpya, Jilumbi, alimwahidi waziri huyo kuwa watahakikisha wanatekeleza maagizo yake, huku akiomba ushirikiano kutoka kwa wateja wa mamlaka hiyo kwa kulipa ankra zao kwa wakati na kutolimbikiza madeni.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shuwasa, Flaviana Kifizi, alisema kwa sasa mamlaka hiyo imeongezewa maeneo mengine matatu ya kutoa huduma ambayo awali yalikuwa yanahudumiwa na Ruwasa, ambayo ni Tinde, Didia na Iselamagazi.

Alibainisha kuwa mamlaka hiyo hukusanya mapato ya wastani wa Sh. milioni 497.892 kwa mwezi, ambapo kiasi hicho cha fedha asilimia tano tu hutumika katika kuongeza mtandao katika maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma ya majisafi na salama.

## Maofisa wawili Nida watumbuliwa

INATOKA UK. 2

wananchi kwa kutopeleka taarifa ili kupata fursa ya kusajili laini zao ambapo zoezi hilo linatarajia kukamilika Januari 20 mwaka huu," alisema.

Lugola alisema serikali inawajali wanyonge, hivyo Waziri wa Mambo ya Ndani ya Ndani ya Nchi, anapambana na watu wanaokwamisha jitihada za serikali.

Waziri huyo pia aliitaka Idara ya Uhamiaji mkoani Ruvuma kufanya kazi usiku na mchana wakishirikiana na Jeshi la Polisi kuwasaka wahamiaji haramu, hasa katika eneo la mpaka wa Tanzania na Msumbiji mkoani humo.

"Ndugu wananchi, toeni taarifa za wahamiaji haramu, itasaidia kuwakamata na pia kushughulikia ipasavyo kwa kuwa watu hao ni hatari kwa uhalifu," aliomba.

Aliongeza kuwa Jeshi la Polisi lipo imara na linaendelea kulinda usalama wa nchi, akidai matukio ya uhalifu mkubwa yamesambaratishwa, na matukio yaliyobaki ni madogo ambayo hayana nguvu katika amani ya nchi.

"Serikali ya Dk. John Pombe Magufuli ipo imara, uhalifu sasa haupo, ujambazi tumeusambaratisha kabisa, kama kuna uhalifu, basi mdogo mdogo tu, huyu kanitukana hivi na vile, lakini matukio ya uhalifu makubwa hayapo nchini, nyie mashahidi na mnaona," alitamba.

Waziri Lugola anaendelea na ziara yake katika mikoa ya kusini na baada ya kumaliza Mkoa wa Ruvuma, anatarajiwa kwenda Mtwara na Lindi.

# Madiwani wambana RAS kukabidhi hospitali yao

**Na Happy Severine,** SIMIYU

MADIWANI wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi, wamemtaka Katibu Tawala wa Mkoa wa Simiyu, Jumanne Sagini, kuwakabidhi Hospitali ya Halmashauri (Somanda) ndani ya siku 20, kwa madai kuwa na malalamiko mengi ya upotevu wa vifaa na mali za hospitali.

Madiwani hao walitoa tamko hilo, jana, katika kikao chao cha kawaida cha baraza kilichofanyika kwenye Ukumbi wa Barideco mjini Bariadi.

Walisema malalamiko mengi na upotevu wa vifaa ndani ya hospitali hiyo yanatokea kwa sababu hospitali hiyo haijarejeshwa rasmi kwao kwa maandishi kama taratibu zinavyotakiwa toka wamkabidhi kuwa hospitali teule ya mkoa.

Akitoa ufafanuzi kwa niaba ya madiwani hao, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Robert Rweyo, alisema wamechoka kusikia kero na upotevu wa vifaa ndani ya hospitali hiyo kwa kuwa wanashindwa kuzitatua kutokana na kutokabidhiwa rasmi.

Alidai kuwa tangu walipoikabidhi hospitali hiyo kwa Katibu Tawala, kumekuwa na malalamiko mengi katika utoaji huduma, upotevu wa vifaa (mabati 70, mashine ya utra sound) na Sh. milioni tatu zilizotolewa na Mbunge Andrew Chenge.

"Upotevu wa vifaa na uwapo wa malalamiko mengi hospitalini hapo umetokea ila tunashindwa kufanyia kazi kwa sababu hatujakabidhiwa rasmi kama utaratibu wa kiserikali unavyoelekeza," alilalamika.

Rweyo alihoji sababu za Katibu Tawala huyo kutowakabidhi hospitali yao kimaandishi wakati tayari hospitali teule ya rufani ya mkoa imeshakamilika na inafanya kazi na wakati anaomba kwao, waliikabidhi kwa maandishi.

"Tunamshangaa sana Katibu Tawala wetu wa Simiyu, sisi mkoa ulipotuomba ile hospitali tuwaazime iwe hospitali teule ya mkoa, tulikubali na tukawakabidhi kwa maandishi, sasa kwanini yeye mpaka sasa hajatukabidhi wakati wana miezi sita wamehamia kwao?

"Tunashangaa sana na tunashindwa kuifuatilia na kutatua malalamiko ya hapo kwani hatujakabidhiwa," alilalamika.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Merczedeck Humbe, alisema waliambiwa wamerudishiwa hospitali, lakini bado hawakabidhiwa kisheria.

Aliongeza kuwa mpaka sasa kinachoendelea ni kuandaliwa kwa nyaraka muhimu ili makabidhiano ya kisheria yafanyike.

Madiwani hao kwa pamoja wameridhia na kupitisha azimio la kumtaka Katibu Tawala wa Mkoa, Sagini, kuwakabidhi hospitali yao ndani ya siku 20 kuanzia jana.



Magari yakipita kwa tabu kwenye shimo kubwa lililopo katika daraja la Mto Ng'ombe, linalounganisha eneo la Kijitonyama Ali Maua na Tandale kwa Mtogole, jijini Dar es Salaam jana. Daraja hilo, pia zimezingirwa na rundo la udongo na takataka zilizosababishwa na mafuriko ya mvua.
**PICHA: JOHN BADI**

# Moto wa nyumba ya kulala wageni wateketeza studio

**Na Ndalike Sonda,** KAHAMA

MOTO unaodaiwa kusababishwa na hitilafu ya umeme, umeteketeza vitu mbalimbali katika nyumba ya kulala wageni ya Samanga A, Mtaa wa Namanga, Kata ya Kahama mkoani Shinyanga.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wilayani Kahama, Inspekta Duma Mohamed, alisema tukio hilo lilitokea jana majira ya saa 10:15 asubuhi, ikidaiwa kuwa chanzo chake ni hita ya maji wakati mmoja wa wahudumu alipokuwa anachemsha maji kwa ajili ya chai. Kamanda Mohamed alisema moto huo umesababisha madhara katika chumba kimoja cha Studio ya M.W ya kurekodi muziki, lakini waliwahi kuuzima na wanaendelea na uchunguzi zaidi.

Aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari kwenye matumizi ya umeme na moto.

Msimamizi wa studio hiyo, William Mwakajia, alisema hafahamu chanzo cha moto huo kwa kuwa wakati tukio linatokea, alikuwa amekwenda kunywa chai na aliporejea, alikuta unawaka katika studio hiyo na vitu vyote vya studio vimeungua.

Tukio la moto unaosababishwa na hitilafu za umeme ni la pili kutokea ndani ya wiki mbili katika mtaa huo, la kwanza likitokea katika nyumba ya jirani na hiyo ya kulala wageni na kusababisha madhara makubwa.




Wadau wa madini ya Tanzanite katika Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, Mkoa wa Manyara, wakipata huduma ya fedha kwenye gari la benki ya NMB inayotembea ndani ya ukuta unaozunguka migodi ya madini ya tanzanite jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Huduma kibenki sasa ukuta wa tanzanite

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

WADAU wa madini ya tanzanite katika mji mdogo wa Mirerani, Simanjiro mkoani Manyara, watafaidika na huduma za kibenki, baada ya benki ya NMB, kuanzisha huduma za kifedha ndani ya ukuta unaozunguka machimbo ya migodi ya madini hayo.

Wakizungumza jana, baada ya gari la kutolea huduma (mobile bank) kufika katika eneo hilo na kuanza shughuli ya humasa za kibenki, wadau hao walishukuru kwa kusogezewa huduma hiyo karibu. Mmoja wa wachimbaji wa madini hayo, Hassan Ally, alisema hatua hiyo ni maendeleo makubwa kwa taasisi ya kifedha kuwajali wadau walioko ndani ya ukuta huo maarufu kwa jina la ukuta wa Rais John Magufuli.

Alisema watatumia huduma hiyo kuweka akiba au kutoa fedha pia aliwataka wadau wengine na ambao hawajafungua akaunti, wafungue ili kuondokana na tabia ya kutembelea na fedha nyingi mfukoni.

Stanley Stephen, mwendesha pikipiki ya abiria (bodaboda), alipongeza hatua hiyo kwa kuwa imewarahisishia kazi wadau hao.

"Hata sisi tutaweka akiba bila kutumia gharama za kwenda kwenye tawi la NMB Mirerani. Tutakuwa tunamaliza mambo yetu ya kibenki ndani ya ukuta wa Magufuli," alisema.

Meneja wa NMB Tawi la Mirerani, Allan Kombe, akizungumza na wadau hao, alisema huduma ya fedha inatolewa rasmi ndani ya ukuta huo, hivyo akawataka wadau hao kutumia fursa hiyo.

Kombe alisema wadau wa tanzanite ni fursa kwao kupata huduma ya kuweka fedha, kutoa fedha na kufungua akaunti kupitia benki hiyo.

Alisema watumishi wa benki hiyo, wamejipanga ipasavyo kutoa huduma, hivyo akawataka kutumia fursa hiyo ya kutembelea huduma za kibenki.

# Wajawazito wapewa elimu maambukizi ya VVU

**Na Allan Isack,** BABATI

WAJAWAZITO wilayani Babati mkoani Manyara, wamepatiwa elimu ya maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto akiwa tumboni.

Elimu hiyo ilikwenda sambamba na kuwaelimisha wajawazito namna ya kumkinga mtoto wakati wa kujifungua endapo mwanamke ana VVU.

Mdau wa maendeleo wa Kata ya Magugu wilayani Babati, Dk. Juma Muna, alijitolea kutoa elimu ya uzazi kwa wanawake wa eneo hilo bila malipo.

Muna ambaye kitaalamu ni daktari wa binadamu, alisema wanawake wajawazito wenye maambukizi ya VVU wakihudhuria kliniki kwa kipindi chote hawawezi kuwaambukiza watoto wakati wa kujifungua.

Alisema watoto watazaliwa salama endapo wa mama waathirika watakuwa wakitumia dawa za kufubaza makali ya VVU pamoja na chandarua ili kukabiliana na malaria.

Hata hivyo, alisema kipindi cha ujauzito mtoto anapokuwa tumboni na wakati wa kujifungua, inatakiwa kulindwa asipate damu ya mama ambayo itamsababishia maambukizi ya VVU.

Aidha, alisema, kinga ya kwanza kwa mwanamke mwathirika na mtoto asiambukizwe ni kumnyonyesha maziwa ya mama kwa miezi sita bila kumpa chakula kingine itamsaidia mtoto kukua vizuri.

"Pamoja na hayo, wajawazito waacheni kunywa pombe au kuvuta sigara. Pia wajikinge na maradhi ya zinaa na wanyonyeshe watoto kwa miezi sita bila kupewa chochote hata maji haitakiwi," alisema Dk. Muna.

Alisema wanawake wengi mkoani Manyara hawanyonyeshi watoto ipasavyo, wengine hunyonyesha watoto mara tatu kwa siku.

Mmoja kati ya wanawake wa eneo hilo, Husna Abdul, alimshukuru Dk. Muna kwa kutoa elimu ya afya bila malipo kwa kuwa imewajengea uwezo zaidi ya awali.

Licha ya kuzungumza hayo, alisema wamepata elimu ya kuwakinga watoto na VVU, namna ya kuwanyonyesha watoto kwa kipindi cha miezi sita ili wawe na afya bora, ambayo itawasaidia kuondokana na ugonjwa wa utapiamlo.

Alisema vyombo vya habari mkoani hapa vimeripoti kuwa asilimia 30 ya watoto wanakabiliwa na utapiamlo kutokana na lishe duni wanayopatiwa.

# Walimu watakiwa kutumia viboko

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro, awataka walimu wa shule za msingi na sekondari jijini Arusha, kutosita kuwaadhibu kwa viboko wanafunzi wenye nidhamu mbaya ili kurejesha nidhamu shuleni jambo litakalosaidia kuongeza ufaulu.

Daqarro ametoa rai hiyo jana, wakati akizungumza na walimu wa shule za msingi na sekondari jijini hapa.

Alisema suala la utii na nidhamu shuleni halina mjadala, hivyo alisema walimu wanao wajibu wa kutumia viboko pale inapolazimika bila kumwonea mwanafunzi.

"Ninacho waomba walimu mrejeshe nidhamu kwa wanafunzi na msikubali kuzoeana nao sana kufanya hivyo, itasaidia kurudisha nidhamu shuleni, lakini msimwonee wanafunzi na kutumia nguvu kupita kiasi wakati mnapotoa adhabu kwa kuwa mnaweza kutenda kosa la jinai," alisema Daqarro.

Mkuu huyo Wilaya, aliagiza kutohamishwa ovyo kwa walimu bila kupewa fedha huku akiwataka walimu wanaoidai serikali kuwa wavumilivu wakati madai yao ya msingi yanashughulikiwa.

Awali, walimu hao kupitia risala yao, iliyosomwa na Katibu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Mkoa wa Arusha, Abraham Kamwela, waliorodhesha matatizo mbalimbali yanayowakabili ikiwamo mazingira ya kazini.

Pia walidai kucheleweshewa kubadilishiwa mishahara kwa kuwa tangu wamepewa barua za mabadiliko ya mishahara bado mabadiliko hayo hayajafanyika ikiwamo suala la kupandishwa madaraja.

Aidha, wameiomba Halmashauri ya Jiji la Arusha kuwakopesha viwanja ili wajenge nyumba za kuishi kwa kuwa baadhi yao wanaishi kwenye mazingira magumu.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Jiji la Arusha Dk. Maulid Madeni, licha ya kuwapongeza walimu hao kwa jitihada zao za kuufanya Mkoa wa Arusha kuwa kinara katika ufaulu kitaifa aliwaomba walimu wazidi kujituma zaidi huku akiwaahidi kuweka mazingira mazuri kazini.

# Kanzi data Chadema kutoa tathmini ya uchaguzi mkuu

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) na Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake (Bawacha) Mkoa wa Kilimanjaro, Grace Kiwelu, amesema uboreshaji wa daftari la wanachama wake litakwenda sambamba na uandaaji wa kanzi data.

Akizungumza na viongozi wanawake ambao ni wanachama wa Bawacha kutoka majimbo saba ya uchaguzi mkoani humo jana, Kiwelu alisema kanzi data hiyo ya wanawake wa Chadema itatoa picha halisi ya watakaokuwa katika mapambano ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Kiwelu aliyasema hayo wakati anahitimisha mafunzo ya wanawake ambao ni wanachama wa Bawacha Kilimanjaro kuhusu mwelekeo wa mwaka wa uchaguzi kwa wanawake.

"Wapigakura wengi maeneo yote ni wanawake, ndiyo maana tunawaomba wakahamasishe wanawake wengine kujiunga na Chadema, huku mkinakili taarifa zao na kuzitunza ili tuweze kutambua wanawake wangapi ni wanachama wetu waliopo tayari kuichagua Chadema ili ishike dola," alisema.

Aliongeza kuwa katika kufikia malengo ya ushindi ya Chadema, Bawacha Kilimanjaro itaboresha mkakati wao wa 'Chadema ni Msingi' na kuhamasisha wanawake wengi kujisajili katika daftari la chama hicho.

"Tunataka kuwainua wanawake kwa kuwajengea uwezo wa kujitegemea kiuchumi, ili kufikia azma ya kauli mbiu yetu ya 'Maendeleo Ni Mwanamke'.

"Tutaratibu mafunzo ya uongozi kwa wanawake na kuhamasisha wanawake wengi kugombea nafasi mbalimbali za uongozi," Kiwelu alitamba.

Pia alisema Bawacha inapanga kuratibu mafunzo ya uongozi kwa wanawake na kuhamasisha wanawake wengi kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

# 'House Boy' jela miaka 30 ulawiti

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

MFANYAKAZI wa ndani wa kiume (house boy), Juma Mwakikoti, mkazi wa Machame Foo wilayani Hai mkoani Kilimanjaro, amehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani, baada ya mahakama kumtia hatiani kwa kosa la ulawiti.

Mahakama ya Wilaya ya Hai jana ilimtia hatiani Mwakikoti mwenye umri wa miaka 30 baada ya kujiridhisha pasipo shaka kwamba alitenda kosa hilo la kumlawiti mwanafunzi wa darasa la sita (15). Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Mkazi wa Wilaya hiyo, Devotha Msofe, alisema mahakama hiyo imeridhika na ushahidi wa mashahidi watano wa upande wa mashtaka ambao wameijenga kesi hiyo na kutoa ushahidi usioacha shaka kwamba mshtakiwa Mwakikoti alitenda kosa hilo wakati akijua ni kosa kisheria.

"Ushahidi wa upande wa mashtaka umefanikiwa kuijenga kesi hii na ushahidi walioutoa watu watano, akiwamo daktari aliyefanya uchunguzi wa kitabibu, ndugu wa mtoto pamoja na Ofisa wa Dawati la Jinsia na Watoto la Polisi, haujaacha shaka ndani yake. Hivyo mahakama hii inakutia hatiani kwa kutenda kosa," alisema.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, Mwendesha Mashtaka aliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa kutokana na kukithiri kwa vitendo hivyo ili iwe fundisho kwa watu wenye tabia kama yake.

Awali ilidaiwa mahakamani hapo na Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Lubulu Mbise, kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo Novemba 5, 2019 katika Kijiji cha Machame Foo na kumsababishia maumivu makali huku akitambua kufanya hivyo ni kosa na kinyume cha kifungu cha 154 (1) (2) Sura ya 16 cha Sheria Kanuni ya Adhabu na marejeo yake ya mwaka 2002.

Ilidaiwa mahakamani hapo kuwa, siku ya tukio mshtakiwa alimshawishi kwa fedha mtoto huyo na kumwingilia kinyume cha maumbile na ikawa ndiyo kila siku anafanya hivyo.

Ili kutekeleza ukatili huo, inadaiwa kuwa mshtakiwa huyo alimrubuni mwanafunzi huyo kuaga kwamba anakwenda kukata majani kwa ajili ya mifugo na ndipo mshtakiwa alikuwa anatumia fursa hiyo kumlawiti.

Wakati wa ushahidi, dada wa mwanafunzi huyo alidai mahakamani kwamba yeye ndiye aligundua kulawitiwa kwa mdogo wake, baada ya kumkuta mdogo wake akiwa na mpira wa kiume (kondomu).

Shahidi huyo wa upande wa mashtaka wakati akitoa ushahidi wake, alidai kuwa baada ya kuona mpira huo wa kiume, alimuuliza mdogo wake na akamwambia wakienda kukata majani ya mifugo kuna kijana huwa anamfanyia mchezo mchafu, kwa kutumia mpira huo.



Ofisa wa Shirika la kiraia la Kwieco, Peter Mashingia (kulia), akihojiana na mmoja wa wazee wa koo, kuhusu ukatili dhidi ya watoto unavyofanyika katika Kijiji cha Merali, Kata ya Sanya Juu, wilayani Siha, Mkoa wa Kilimanjaro jana. Mradi wa hamasa kuhusu mpango kazi wa kitaifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya watoto wa kike katika wilaya hiyo unaotekelezwa na shirika hilo. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Washtushwa kasi ukataji miti

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SHIRIKA la Roots & Shoots, linalofanya kazi ya upandaji miti na ulinzi wa hifadhi ya mazingira katika Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, limeeleza kusikitishwa na uharibifu wa vyanzo vya maji unaoendelea katika baadhi ya mitaa, ambako watu wasiojulikana wamevuna miti kinyume cha sheria.

Mhifadhi wa Mazingira wa Shirika hilo, Dominiki Osoki, alisema miti hiyo imeng'olewa katika mashamba yanayopakana na vyanzo vya maji na hasa kwenye mabonde ya hifadhi ya maji.

Akizungumza na Nipashe jana, Osoki alitaka serikali ichukue hatua za kutoa elimu kwa wakulima wenye mashamba yanayopakana na vyanzo hivyo, ili kuzuia uharibifu huo kuendelea zaidi na kusababisha athari mbaya katika miaka ijayo.

"Katika tathmini ya uharibifu wa chanzo cha maji Msiriwa, tumebaini jumla ya miche 45 ya miti aina ya mikufi, mihaa na misesewe huko katika Kijiji cha Njari imeng'olewa. Hifadhi ya Mto Msiriwa kumepandwa mahindi na maharage.

"Pia miti sita imepunguzwa wakati ni kosa kisheria kufanya shughuli zozote za kibinadamu ndani ya mita 60 kutoka kwenye chanzo cha maji na kimsingi miti iliyoharibiwa kwa kung'olewa au kuvunwa iko chini ya sentimeta tano," alibainisha.

Kwa mujibu wa Osoki, shirika hilo liliweka mkakati maalum wa kupanda na kuilinda miti yote iliyopandwa katika Mto Rau, Chemchem ya Mchumu, Korongo la Njari, Chemchemi ya Kariwa na Chemchem ya Mbora.

Maeneo mengine ni pamoja na Zahanati ya Rononi, Zahanati ya Mmeu, Chemchem ya Owa, Msuni kwa Msoka, Zahanati ya Fumbuni Uru Kaskazini na Mrawi Shinga kwa Msoka.

Pia yamo maeneo ya Chemchem ya Makewa, Mto Ngomberi, Chemchem ya Leoni Chuwa, Chemchem ya Siaka Njari, Chemchem ya Mbuo, Chemchem ya Mawela, Mrupanga Rau, Mto Lukaranga na Bonde la Chombo.



## HABARI DODOMA



Mwananchi akipita jirani na rundo la takataka zilizotelekezwa bila ya kuzolewa kwa muda mrefu sasa, katika Soko la Bonanza, eneo la Chamwino, jijini Dodoma jana, kitendo kinachosababisha kero kwa wakazi wa eneo hilo, kutokana na harufu kali inayoweza kuhatarisha usalama wa afya zao. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Waziri ataka huduma saa 24 maduka kubadili fedha

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Atashasta Nditiye, ameliagiza Shirika la Posta Tanzania, kuhakikisha linafungua maduka ya kubadilishia fedha za kigeni kwa saa 24 katika miji mikubwa nchini.

Nditiye alitoa agizo hilo juzi jijini hapa wakati akifungua mkutano wa siku tatu wa Baraza la Wafanyakazi na Postamasta Mkuu wa Shirika hilo.

Alisema ni lazima kutumia fursa ya kufungwa kwa benki zinazotoa huduma hizo kwa kutoa huduma ya kubadilishia fedha saa 24, hususan kwenye miji mkubwa kama Dodoma, Arusha, Mwanza na Dar es Salaam.

"Kuna siku nilitaka kubadilisha fedha hapa Dodoma, nikakuta maduka ya posta yamefungwa, benki zimefungwa, hivyo ni lazima sisi tubadilike na kutumia fursa ya benki zingine kutofungua siku za mwishoni mwa wiki, sikukuu na usiku kwa kuhakikisha Shirika la Posta Tanzania likatoa huduma hiyo kwa saa 24 kila siku," aliagiza.

Nditiye pia alilitaka shirika hilo kuhakikisha linaongeza wigo wa huduma kwa kupeleka kwa wananchi na hususani katika wilaya ambazo shirika hilo halina ofisi.

"Huu ni wakati wa Shirika la Posta kufanya biashara kubwa ya huduma za posta, kutuma fedha na kubadilisha fedha, nafasi na uwezo huo mnao.

"Mjue si kila mtoa huduma ya kusafirisha barua, vifurushi na vipeto anatakiwa kubeba kila nyaraka, kwa vile ninyi ni shirika la serikali, mna fursa ya kufanya biashara hata ya kubeba nyaraka nyeti kwa sababu mnaaminika," alisema. Nditiye pia aliwakumbusha watumishi wa shirika hilo kuendelea kusimamia uwajibikaji kwa viongozi na watumishi wa kanda zote ndani ya shirika kwa kujenga nidhamu ya kazi, kujituma, kuheshimu kanuni na taratibu, kuongeza ubunifu na kufanya kazi kwa ufanisi.

# DC aonya wazazi wanaowaficha wanafunzi kidato cha kwanza

**Na Ibrahim Joseph,** KONGWA

MKUU wa Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma, Deogratius Ndejembi, amewataka wazazi kuhakikisha wanawapeleka shule watoto waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu wa masomo 2020 kabla ya wiki ijayo.

Alitoa agizo hilo jana wakati wa ziara yake ya kukagua miundombinu ya majengo ya madarasa ili kuhakikisha wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wanaanza masomo.

Ndejembi aliwataka wazazi kuhakikisha wanawapeleka watoto wao shule kabla ya wiki ijayo ili kuwahi ratiba yao ya masomo.

"Sitahitaji kisingizio chochote cha mzazi atakayemchelewesha mtoto wake shule, nimezunguka kwenye baadhi ya shule za wilaya yetu, nimejiridhisha kuwa watoto wote wataingia madarasani katika msimu huu," alisema.

Alisema lengo la wilaya hiyo ni kuhakikisha watoto wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu, wanapelekwa shule. Aliwataka baadhi ya wazazi ambao bado hawajakamilisha kuwanunulia watoto wao mahitaji, kuhakikisha wanafanya hivyo haraka mwisho wa wiki hii ili wiki ijayo waripoti shuleni.

Aliongeza kuwa serikali imeamua kutoa elimu bure kwa kuwalipia wanafunzi gharama za ada na zingine ili wapate elimu bila kisingizio chochote.

Alisema awali walikuwa na tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa 37, lakini kwa kutumia nguvu za wananchi na baadhi ya wadau wa elimu, wamefanikiwa kulitatua.

Alibainisha kuwa katika maeneo mengine, kulikuwa na upungufu wa ofisi za walimu na kuzifanya vyumba vya maabara kuwa ofisi ili kuhakikisha wanafunzi walichaguliwa wanaingia darasani, lakini sasa wametatua pia tatizo hilo. Alimshukuru Spika wa Bunge na Mbunge wa Kongwa, Job Ndugai, kwa kutoa kiasi cha Sh. milioni sita kwa kila shule zilizokuwa na tatizo uhaba wa vyumba vya madarasa na kufanikiwa kukamilisha vyumba hivyo.

Alisema kutokana na juhudi za mbunge huyo, wanaendelea kuhakikisha kuwa wanamaliza uhaba wa vyumba vya madarasa mpaka kwa shule za msingi zilizoko katika wilaya hiyo.

Pia alisema kuna majengo 292 yanayoendelea kujengwa katika wilaya hiyo kwa shule za msingi na sekondari kwa nguvu ya wananchi.

Alizitaja baadhi ya shule zilizokuwa na uhaba wa vyumba vya madarasa kuwa ni Chitego na Kibaigwa, lakini baada ya ushirikiano huo wa mbunge, walifanikiwa kuwasaidia wanafunzi hao kuingia madarasani na kuanza masomo.

# Ataka vibanda vya mitaroni vivunjwe

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAFANYABIASHARA kwenye masoko mbalimbali jijini Dodoma, waliojenga vibanda vyao vya biashara kwenye mifereji inayopitisha maji, wametakiwa kuviondoa ili miundombinu hiyo ipitishe maji.

Agizo hilo lilitolewa jana na Ofisa Masoko wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, James Yuna, alipozungumza na wafanyabiashara hao kutokana na baadhi yao kujenga kwenye maeneo ya miundombinu inayopitisha maji na kusababisha kuziba.

Alisema kutokana na hali hiyo, wafanyabiashara wote ambao wamejenga vibanda juu ya mifereji hiyo iliyojengwa kwa ajili ya kupitisha maji kwenye masoko, ni lazima waondoke ili kuondokana na adha inayojitokeza kwa kipindi hiki cha mvua.

"Hakuna sababu ya kuwapo kwa tope hilo na kuzagaa kwa takataka wakati kwenye masoko hayo kuna mifereji ambayo tayari imeshatengwa kwa ajili ya kupitisha maji.


"Tatizo lililopo kuna baadhi ya wafanyabiashara wamejenga juu ya mifereji hiyo na kusababisha kuziba, na maji hayo kukosa sehemu ya kupita na badala yake yanasambaa," alisema.

Hata hivyo, ofisa huyo alisema Halmashauri ya Jiji bado inaendelea kufanya ukarabati wake ndani ya masoko yote kuhakikisha miundombinu yake inakuwa rafiki kwa wafanyabiashara na watumiaji wake.

Alitaja baadhi ya masoko ambayo tayari ukarabati wake umeanza kuwa ni pamoja na Soko la Sabasaba, ambalo sehemu ya stendi ya daladala imekarabatiwa kwa kuwekwa kifusi na kusambazwa, Soko la Bonanza, Kikuyu na Changombe ambayo tayari yamejengewa mapaa na kufanya wafanyabiashara na wateja kufanya shughuli zao bila bugudha.

Yuna aliwataka wafanyabiashara kufanya shughuli zao kwa kufuata sheria na kanuni zilizowekwa na Halmashauri ya Jiji.

Alisema hali hiyo ni kutokana na baadhi yao kupanga biashara kwenye maeneo yanayohatarisha maisha yao na watumiaji wa maeneo hayo kama vile wapiti njia na waendesha vyombo vya moto.






Baadhi ya vijana wa Umoja wa Vijana wa CCM, wakiwa katika matembezi ya kuenzi Mapinduzi ya Zanzibar, yaliyopokelewa na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan (hayupo pichani), katika Viwanja vya Mapinduzi Square, Michezani mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Makamu Rais awaonya vijana CCM

**Na Rahma Suleiman,** UNGUJA

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amewataka vijana wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) kuwa wazalendo wa nchi yao na kuacha papara za kutaka kuwa viongozi serikalini au katika chama.

Samia aliyasema hayo alipozungumza katika hafla ya kupokea matembezi ya umoja huo, jana, kusherehekea Mapinduzi ya Zanzibar ambayo kilele chake ni kesho.

Alisema vijana wa sasa wamekuwa na haraka ya kutaka kuwa viongozi badala ya kuwa na umoja na uzalendo kwa nchi.

Alisema anafahamu UVCCM ni tanuru la kuwapika viongozi, lakini linapaswa litumike vyema kuwapika vijana hao na muda utakapofika, serikali itawapa fursa za uongozi."UVCCM ni tanuru la kuwapika vijana, lakini mmekuwa na migogoro mingi kwa sababu ya tamaa ya kutaka uongozi," Samia alibainisha.

Aliutaka umoja huo kuachana na fitina na majungu ambayo alisema hayatauimarisha umoja wao.

Aliwataka vijana hao kupendana na kuwa wa umoja na kuhakikisha wanajitokeza kwa wingi kujiandikisha katika daftari la wapigakura wakati ukifika.

# Balozi Iddi ataka elimu Mapinduzi

**Na Rahma Suleiman,** UNGUJA

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema Wazanzibari wanapoadhimisha Miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar, lazima wale walioshuhudia wajikumbushe na kizazi kipya kisome historia ili kujua vyema dhamira yake.

Amesema Chama cha Afro Shirazy Party (ASP) kilikuwa kikishinda kila mara kwenye uchaguzi wa vyama vingi wakati kikipigania kujikomboa kutoka katika makucha ya wakoloni.

Balozi Iddi aliyasema hayo alipozungumza na wananchi wa Kijiji cha Bwejuu baada ya kuzindua majengo mawili ya Shule ya Charity kwa ajili ya madrasa na bweni.

Alisema dhamira hiyo ya ASP ndiyo iliyosababisha wananchi wa Zanzibar chini ya uongozi wa marehemu Abeid Aman Karume, kuondoa mzizi wa fitina Januari 12, 1964 ili kurejesha heshima, haki na usawa kwa wananchi walio wengi wa visiwa vya Unguja na Pemba waliyoikosa kwa zaidi ya karne mbili.

Alisema wakati Watanzania wanaadhimisha miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar, watoto wa visiwa hivyo lazima wadhamirie kusoma kwa bidii kwa kuwa tayari wameshatengenezewa fursa na mazingira ya kufanya hivyo.

Balozi Iddi alisema kazi inayowakabili kwa sasa watoto wote kusoma kwa nguvu zao zote katika malengo ya kwenda sambamba na mabadiliko makubwa ya sayansi na teknolojia yanayoikumba dunia kwa wakati huu.

"Serikali Kuu inaendelea kutengeneza fursa katika kila kada na kilichobakia ni juhudi za wanafunzi wenyewe katika kufikia dhamira hiyo muhimu katika mustakabali wa maisha yao ya baadaye," alisema.

Aliongeza kuwa uwezo wa wanafunzi kufikia malengo hayo upo kwa kuwa mazingira ya kupata taaluma katika ngazi hadi udaktari yanapatikana Zanzibar ndani ya vyuo vikuu vilivyoanzishwa.

Alisema elimu ni silaha njema inayoweza kutumiwa wakati wowote licha ya upungufu wa ajira uliopo nchini kwa sasa aliodai unatokana na ongezeko kubwa la wasomi wanaomaliza elimu ya sekondari na vyuo vikuu.

Akitoa taarifa ya kitaalamu kuhusu mradi huo wa kijamii, Katibu Mkuu Wizara ya Eimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Idriss Muslim Hijja, alisema zaidi ya Sh. milioni 682 zimetumika kugharamia mradi huo.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, alisema ujenzi wa bweni ni moja ya mikakati bora inayowajengea wanafunzi kupata muda wa ziada wa kujisomea.

Mradi wa Shule ya Charity Bwejuu ulioanzishwa na wananchi wenyewe mwaka 2014 ukianza na wanafunzi 25, ulilenga kuwarejesha masomoni watoto walioacha shule, yatima na watoto wenye mahitaji maalum.

# 'Msajili amulike uchochezi 2020'

**Na Mwandishi Wetu,** UNGUJA

MSAJILI wa Vyama vya Siasa nchini, ametakiwa kuangalia Sheria ya Vyama vya Siasa ya Mwaka 1992 ili kuwabana baadhi ya viongozi wa kisiasa wanaotoa kauli zinazoashiria chuki na uhasama kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Rai hiyo ilitolewa jana na Waziri Asiye na Wizara Maalum wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Juma Ali Khatib, wakati wa uzinduzi wa jengo la hospitali ya kinamama na watoto huko Kiboje Wilaya ya Kati Unguja.

Alidai wapo baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa tayari wamepoteza nyadhifa zao, lakini wamekuwa wakitoa kauli za chuki kinyume cha sheria hiyo.

"Katika Sheria ya Vyama vya Siasa msemaji wa chama ni mwenyekiti au katibu mkuu wa chama, kuna huyu mwenzetu anajiita mshauri wa chama huku akichukua jukumu la kutoa kauli za chuki na uhasama dhidi ya viongozi wa vyama vya siasa, uwezo huo ameupata wapi?" Alihoji.

Khatib, ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Ada Tadea, alidai amesikitishwa na matamshi ya baadhi ya viongozi wa kisiasa visiwani Zanzibar kuhusu kile alichokiita kushawishi na kujenga hamasa kwa vijana kuwa tayari kutumia silaha za jadi kama watachokozwa.

Alimpongeza Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein kwa kutekeleza ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015-2020 kwa kupiga hatua kubwa katika maendeleo ya sekta za elimu na afya mijini hadi vijijini.

Alisema siri ya mafanikio hayo ni kuwajumuisha viongozi mbalimbali katika kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kutoa fursa kwa wanasiasa kujenga nchi.

"Tunampongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein kwa busara zake na hekima katika kuongoza nchi kwa kuzingatia demokrasia na utawala bora," alisifu.

Aliwataka wananchi wa Kijiji cha Kiboje kuzitumia huduma za kinamama kwa ajili ya kujifungua salama ili kuepuka vifo vya mama na mtoto.

Alisema mikakati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kupunguza vifo hivyo ikiwa ni sehemu ya kutekeleza Malengo Endelevu ya Dunia.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Shamata Khamis Shaame, alisema ujenzi wa kituo hicho umegharimu Sh. milioni 381.

Alisema hiyo ni sehemu ya mikakati ya kutekeleza dhana ya ugatuzi kufikisha huduma muhimu kwa wananchi, hasa wa vijijini.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kutekeleza malengo ya Mapinduzi ya Januari 12, 1964 kwa kutoa huduma za afya bure kwa makundi yote, wakiwamo wanawake na watoto," alitamba.



**ROMA**

Soma UK.14

JUMAMOSI JANUARI 11, 2020



# UFALME WATIKISIKA

## PRINCE HARRY, MEGHAN KUISHI USWAHILINI

Soma UK.16

BASI SAWA



## Roma ashindwa kunusuru ndoa ya Stamina

HABARI ya mjini kuwa ni wimbo wa Stamina unaoitwa 'Usiwaze' ambao inaaminika ni stori ya kweli inayohusu machungu ya ndoa yake na aliyekuwa mke wake.

Hata hivyo, Rapa Roma Mkatoliki, ambaye pia alikuwa msimamizi wa harusi hiyo, amefunguka kwamba kila kitu kilichoimbwa ni ukweli na kwamba hata yeye alijaribu kuiokoa, lakini ilishindikana.

''Huo wimbo kila kitu ni stori ya kweli, mimi kama msimamizi wake na mlezi wake wa ndoa, nimejaribu kuweka sawa kwa kuweka vikao vingi kusuluhisha lakini ilifika mahali nimeshindwa na mkewe aliondoka toka Machi mwaka jana," amesema Roma.

Mwaka 2020 unaonekana umeanza kwa wasanii mbalimbali kutoa machungu yao kuhusu kuwapotoza wapenzi wao.



## Mabeste naye kumbe yupo singo

Msanii mwingine aliyeamua kueleza ukweli kuhusu maisha ya ndoa ni mwanamuziki wa Bongo Fleva, Mabeste, ambaye amesema ameachana na mke wake kwa muda wa mwaka mmoja.

"Tangu nimeachana na mke wangu umepita karibia mwaka mmoja sasa, naendelea kufanya vitu ambavyo nilikuwa nimepanga, nipo sawa," amesema.

Amesema kuhusu malezi ya mtoto anaendelea kutoa kutokana na kuwa na umri wa kukaa na mama yake ili kupata uangalizi wa karibu.



## SIKINDE WAMKARIBISHA BENO VILLA KWA SHOO KALI

BENDI ya kongwe ya muziki wa dansi, Mlimani Park Orchestra, imemrejesha kundini mtunzi na mwimbaji nguli, Beno Villa Anthony na wamepanga kumtambulisha rasmi siku ya kesho.

Shoo hiyo ya kumkaribisha itafanyika katika ukumbi wa Equator Grill, uliopo Mtoni kwa Aziz Ally, Temeke jijini Dar es Salaam.

Wakizungumzia tukio hilo, Hamis Milambo ambaye ni mmoja wa viongozi wa bendi hiyo, amesema Beno Villa, amerejea baada ya kuondoka kipindi kirefu.

Ameongeza kuwa, onyesho hilo litakuwa maalum kwa kumkutanisha na wadau na washabiki wa Sikinde.

Alisema, kurejea kwa mwanamuziki huyo kumezingatia sababu mbalimbali, lakini kubwa ni mkakati wa kuiboresha bendi hiyo.

"Ni kweli, Beno Villa amerejea rasmi kundini na tayari Sikinde imepanga kufanya mabadiliko makubwa na kuingia katika mfumo wa taasisi ili tuweze kujiendesha kwa ufanisi."

## INSTA-TWITTER





**Unapopata** nafasi ya kumjali na kumthamini mtu, fanya kwa moyo wote. siyo mpaka umpoteze ndiyo ukumbuke kumthamini na kumpenda - **Shamsa Ford.**



**Usiruhusu** mawazo mabaya yakitawale kichwa chako ... Wakisema huwezi mwambie nyie sio Mungu, wakisema umechanganyikiwa waambie hanishtui - **Harmonize.**



## Mashabiki wamkingia kifua Harmonize

MASHABIKI wa mwanamuziki wa Bongo Fleva, Harmonize, wamemtetea msanii huyo wakisema wanaodai kuwa ameiba wimbo wanataka kiki za bure.

Hivi karibuni kumeibuka mjadala katika mitandao nchini Kenya baada ya kudaiwa kuiba shairi la wimbo 'Inauma' wa Stivo Simple Boy.

Baada ya kutokea malalamiko hayo, mashabiki wa mwanamuziki huyo walikuja juu wakidai Wakenya hao wana nia ya kumrudisha nyuma kimuziki na kumtaka kusonga mbele.

"Harmonize hayo madai ya kuiba wimbo usiweke akilini, hao Wakenya wanataka kiki za bure tu, komaa kwa kupika vibao vingine, wacha waseme na mwisho watanyamaza," alisema shabiki mmoja katika akaunti yake ya Instagram.




@burudanitele

**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**



# SIRI NZITO BABA WA MTOTO WA TAUSI AFICHWA

MWIGIZAJI wa filamu za Bongo Muvi, Tausi Mdegela, amewashtua mashabiki wake baada ya kutoa taarifa ya kujifungua mtoto wa kike.

Tausi ambaye amepata umaarufu kutokana na kuwa na kimo kifupi, alijifungua mapema wiki hii na taarifa zake kusambaa kwa kasi katika mitandao ya kijamii.

Hata hivyo, kitendawili ambacho watu hawajapata jibu ni nani baba wa mtoto huyo?

Tausi mwenyewe amesema kitendawili hicho kitakuwa kigumu kupata jibu lake, baada ya yeye mwenyewe kuamua kuweka suala hilo kuwa siri kutokana na watu wengi kuonyesha mawazo hasi kuhusu maumbile yake.

"Siwezi kumtaja baba wa mtoto wangu, naogopa yakamkuta maneno ya kukatisha tamaa kama ninayopewa mimi. Lakini namshukuru Mungu kwa kunipa zawadi hii ya mtoto," amesema Tausi.

Amesisitiza kwamba hata suala la ujauzito wake alishauriwa kukaa mbali na mitandao ya kijamii ili kuepuka midomo ya watu.

"Mara nyingi watu wanaona maumbile yangu siwezi kufanya vitu ambavyo wenzangu wanaweza, nilishauriwa kuwa mbali wakati nikiwa na ujauzito kwa kuhofia watu wanaonitazama vibaya." Amesema Tausi.

## INSTA-TWITTER



Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**Mwaka** 2020 tayari kwa kupiga kazi, Ehee Mungu waongoze na kuwafungulia milango yote ya kheri na baraka kwa wapambanaji wote, Ameen - **Rose Ndauka.**



**Mwaka** huu atucheki na kima ukizinguwa tunakuzingua. Mnunoo 'heavy' achana na ndala zangu we angalia picha - **Amber Lulu.**



**Hongereni** kinamama mnaowalipia watoto zenu ada, wakati baba zao wapo mjini wanazurura. Halafu mkiambiwa watoto sio wenu ole wenu mlete vurugu - **Flora Mvungi**.

# Kuumbe!



# UFALME WATIKISIKA

## PRINCE HARRY, MEGHAN KUISHI USWAHILINI

TAMKO la Mwanamfalme Harry na mkewe Meghan kuachana na kujihusisha na shughuli za kifalme limeleta mshtuko duniani kote.

Baada ya kutolewa tamko hilo juzi, ufalme wa Uingereza ulipata hofu na kuelezea jinsi walivyoshtuka mara wanandoa hao waliposema kuachana na shughuli za kifalme.

Kasri la Buckingham limetoa taarifa kwamba limehuzunishwa na maamuzi hayo na kusema haikuhusishwa, na wala haikuwa na taarifa zozote za awali kuhusu maamuzi ya wanandoa hao.

BBC imebaini kuwa si malkia wala mwana mfalme William au waandamizi wengine katika falme hiyo walijulishwa hatua hiyo.

Kasri la kifalme limesema kuwa suala hili ni gumu na wamelipokea kwa mshtuko mkubwa.

Mwandishi wa zamani wa BBC masuala ya kifalme Peter Hunt, amesema amepata hofu kutokana na taarifa hiyo.

"Mara nyingi huwa ninapata hofu kutumia neno 'haijawahi kutokea' ingawa sina mfano ambao ninaweza kufikiria kusema kuwa familia ya kifalme iliwahi kujisafisha katika jambo kama hili kwa umma."

Katika maelezo yao, Harry na Meghan ambaye ni mcheza filamu mwenye asili ya Afrika, walisema kuwa walifikiria uamuzi huo kwa muda mrefu na kufanya maamuzi hayo miezi mingi iliyopita.

Harry na Meghan wamepanga kugawa muda wao kwa nusu kuishi Marekani na nusu Uingereza, kuendelea kumtumikia malkia na kujihusisha na shughuli za kifalme.

"Maamuzi hayo yataturahisishia kumlea mtoto wetu katika makuzi ya utamaduni wa kifalme, na kuipa fursa familia kuangalia hatua inayofuata," walisema wapenzi hao.

Msemaji wa zamani wa malkia Dickie Arbiter, emesema kuwa hafahamu ni namna gani wataweza kugeuza mipango yao.

"Hii ni kama ndoto, kuna suala la usalama nani atatoa ulinzi kwao?

"Je, ni nchi gani itawapa ulinzi wa kifalme? Je, ni Canada au nani atalipia?" Alihoji

Hatua hii inakuja baada ya mwezi Oktoba mwaka jana mwanamfalme Harry na mkewe walilalamika kuingiliwa maisha yao kwa kufuatwa na vyombo vya habari kwa kivuli kuwa wanatoka katika familia ya kifalme.

Katika ukurasa wake wa Instagram, Harry na mkewe wamejitetea kwamba wameifikia hatua hiyo baada ya kuwa na majadiliano ya ndani kwa miezi kadhaa.

Hata hivyo, maamuzi yao yamepingwa vikali ikidaiwa walistahili kupewa kwanza idhini ya jambo hilo kabla ya kutoa taarifa.

Malengo yao mengine ya kujiondoa katika shughuli za moja kwa moja za kifalme, ni kutaka kufanya kazi za kawaida katika kuendesha maisha yao ya kila siku badala ya kutegemea mapato yatokanayo na nafasi zao za kifalme.

Ingawaje wamesisitiza kwamba bado wataendelea kumuunga mkono malkia na ufalme kwa ujumla.

Katika maelezo yake kupitia ukurasa wa Instagram mwana mfalme Harry ameomba waruhusiwe kama walivyoamua yeye na mkewe.

Baadhi ya wachambuzi wa masuala ya kifalme nchini Uingereza, wamekaririwa wakibeza hatua hiyo ya Harry na mke wake, wakieleza wamekiuka taratibu kadhaa za namna ya kuishi kama mwana mfalme.

# Hakuna kuremba 2020

**Na Adam Fungamwango**

KUNA watu hawarembi bwana! Mwaka 2020 umeingia tu, tayari kuna baadhi ya wasanii wameshatoa ngoma zao ambazo ingawa ni kwa muda mfupi tu, lakini zimeanza kuwa gumzo kwa mashabiki.

Mwezi huu huu wa Januari, kuna ngoma zimetoka ambazo zimewafanya mashabiki kuachana na kuzizungumzia zile za mwaka uliopita, badala yake mazungumzo ni hizi mpya.

Kumbe wakati watu wanasherehekea sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya, kuna baadhi ya wasanii walikuwa studio wakitengeneza ngoma zao na kutaka mwaka 2020 waingie kivingine, tena kwa kishindo.

**Mbosso - Atte**

Msanii Mbosso, zao la Yamoto Band, ametambulisha ngoma yake mpya iitwayo 'Atte'.

Ameitoa Januari 6 mwaka huu. Ni wimbo wa mapenzi ambao tayari hadi jana Ijumaa Januari 10, ulikuwa umeshaangaliwa na watu 582,959.

**Ommy Dimpoz ft Nandy - Kata**

Ommy Dimpoz, naye ni mmoja wa wasanii ambao mwanzoni tu mwa mwaka 2020, ameibuka na kuitambulisha ngoma yake mpya ambayo ameipa jina la 'Kata'. Ni wimbo ambao amemshirikisha msanii wa kike Nandy. Ni ngoma ya maudhui ya mapenzi ambayo imepigwa na kuimbwa kwa mtindo wa 'ragamuffin'.

Msanii huyo ameitambulisha ngoma yake hiyo Januari 3 mwaka huu na tayari kwenye mtandao wake na imeshatazamwa na watu 993,057.

**Harmonize - Hainishtui**

Haikutegemewa kama msanii mkubwa kama Harmonize atawahi kutoa ngoma mapema tu siku za mwanzoni za mwaka 2020. Ilitegemewa angesubiri kwanza wengine watoe kwa sababu yeye ni staa, lakini haikuwa hivyo.

Lakini siku tatu tu baada ya mwaka mpya, akatambulisha ngoma yake mpya aliyoipa jina la 'Hainishtui'. Labda kwa sababu za kibiashara, ameitoa kwenye audio na si video, na tayari kwenye mtandao wake umeshatazamwa na watu 758,372, hapo bado ile ya video.

Huu si wimbo wa mapenzi, bali msanii anasema maneno na vitisho vya watu havimshtui.

'Wenzako watakuroga, au na wewe umeshaoga, maana hauna woga. Wapo anaosema Konde atapotea, wenzako wanakuchukia, tena wamepanga kukubania, hainishtui, wakinifunika mimi nitawafunua...' Ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye ngoma hiyo.

**Roma Mkatoliki - Mkombozi**

Ni ngoma ambayo baadhi ya watu wanadai kuwa haikutakiwa kuwa kwenye bongo fleva bali Gospel.

Ni wimbo ambao unamhusisha mtu mwenye matatizo mengi kwenye maisha, anayemwomba Mungu amsamehe na kumpunguzia shida za duniani. Alikwenda mahasubu lakini ndugu hawakwenda kumuona, aliporejea hakuwa na kinyongo, aliwabusu, lakini wakasema amewasonya. Huku anadaiwa vikoba, kule anadaiwa rejesho, kiasi cha kwenda kujificha Goba. Amekwenda kwa waganga na kuvunja nazi njia panda, lakini wapi, lakini kwa sasa amemrudia Mungu na anamuomba amalize shida zake. Ngoma hii iliyotoka Januari 3, imeshasikilizwa na watu 463,392.

**Stamina - Asiwaze**

Alhamisi ya Januari 9, Stamina ametambulisha ngoma yake mpya iitwayo 'Asiwaze'. Ni wimbo ambao ameimba kwa hisia kali. Watu 382,737 wameshaitazama ngoma hiyo.

Ni ngoma ya masikitiko ambayo Stamina anaimba kuhusu ndoa ndoano.

Alalamika kuwa hata pete yake ya ndoa ameshaenda kuiuza kwa sonara na kurudisha nusu hasara aliyotumia kwenye ndoa. 'Ndoa inaweza kukufanya ulewe bila kunywa pia. Ile suti niliyovaa ya nini?

'Mwambieni yule dogo aliyechezea klabu ya Simba, kutembea na mke wangu, asijione kama ameshinda, nimeshakula, sasa ruksa kutoa vyombo...' Ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye ngoma hiyo.



IMETOKEA

# Maelfu ya ngamia kuuawa kisa wanakunywa maji mengi

MAELFU ya ngamia kusini mwa Australia watauawa kwa risasi kutoka kwenye helikopta kutokana na kuwapo kwa joto kali na ukame.

Zoezi hilo la siku tano limeanza Jumatano wiki hii, jamii ya eneo hilo imeripoti kuwepo kwa makundi makubwa ya ngamia kuharibu miji na majengo.

"Wanaambaa mitaani wakitafuta maji ya kunywa. Tunahofu kuhusu usalama wa watoto", anasema Marita Baker, ambao wanaishi kwenye jamii ya Kanypi.

Baadhi ya wanyama pori pia watauawa.

Maofisa watakaofanya kazi hiyo wanatoka katika idara ya mazingira na idara ya maji.

Imeelezwa kuwa kutokana na hali ya ukame, ngamia wamekuwa tishio kwenye jamii hivyo na inahitaji udhibiti wa haraka.

Jamii zinazoishi karibu na makazi ya ngamia hao, wamesema wamekuwa wakiishi katika mazingira magumu, kwa sababu ngamia hubomoa uzio, huzunguka nyumba wakijaribu kupata maji kupitia maji yanayodondoka kutoka kwenye viyoyozi.

Joto kali na ukame kumesababisha moto wa nyika nchini Australia kwa kipindi cha miezi kadhaa, lakini hali ya ukame ya nchi hiyo imekuwapo kwa miaka kadhaa.

Ngamia hawana asili ya Australia, walipelekwa nchini humo na walowezi kutoka India, Afghanistan na mashariki ya kati katika karne ya 19.

Ngamia hao huharibu uzio, vifaa vya shamba na makazi, na pia hunywa maji yanayohitajika kwa matumizi ya watu katika eneo hilo.

Pia hutoa gesi ya methane, gesi ambayo inachangia mabadiliko ya hali ya hewa.

Maeneo ya mashariki na kusini mwa Australia yameharibiwa vibaya na wanyama wengi wameuawa kwa moto.

Nchi hiyo imekuwa ikikumbwa na joto kali katika kipindi cha miongo ya hivi karibuni na hali inatarajiwa kuendelea.

Wanasayansi wametahadharisha kuwa hali ya joto kali, na ukame utachangia matukio ya moto mara kwa mara na kuleta madhara.






# Penzi la Giza Ubaya hata shetani anashangaa

**Na Adam Fungamwango**

AMA kweli ubaya hauna posho na roho mbaya haijengi. Duniani kuna watu wenye tabia ya kuwachukia wenzao bila sababu, lakini hawanufaiki na chochote.

Wapo kwenye tabia ya kuwafanyia ubaya wenzao kwa sababu ambazo hazieleweki. Hawafanyi hivyo labda kwa kulipiza kisasi la hasha, bali wao wanaona furaha kumfanyia mtu ubaya.

Inafika wakati binadamu anafanya ubaya hadi shetani anashangaa.

Hali hii inajionyesha kwenye filamu ya Penzi la Giza ambayo imechezwa na baadhi ya wasanii maarufu ambao ni Issa Mussa Cloud 112, Irene Paul Asia Buheke, Queen Njau na wengineo wengi.

Mr. Nabil ni bosi kwenye kampuni moja kubwa jijini Dar es Salaam. Chini yake ana baadhi ya wasaidizi ambao wanakitaka cheo chake kwa udi na uvumba, licha ya kwamba anafanya kazi zake vizuri tu.

Bosi msaizidi ndiye anayekitaka cheo hicho akishirikiana na baadhi ya wafanyakazi. Msaidizi huyo wa bosi Nabil anafanya hila mbalimbali za kumkwamisha kazi Nabil aonekane hajui, lakini inashindikana, kwani wamiliki au wakuu wa bodi wanaona anafanya kazi nzuri, hivyo wanampongeza kwa kazi nzuri.

Baada ya kuona upande huo unashindikana, bosi msaidizi anaamua kutumia njia za giza kufanikisha jambo lake. Anaamua kwenda kwa waganga wa kienyeji ili wafanye kila mbinu, ama ya kumwondoa kwenye kiti chake cha ubosi mkuu, au ikishindikana kumuua kabisa.

Mganga anatengeneza jini ambalo linatumika kwa ajili kwenda kummaliza Cloud ambaye amecheza kama Nabil.

Jini hilo linatengenezwa kuwa msichana mzuri ambaye nia ni Cloud aingie mkenge na kumpenda, halafu ammalize. Kwa bahati mbaya au nzuri haiwi hivyo.

Irene Paul ambaye alicheza kama jini, baada ya kuona utanashati na Cloud anabadili mawazo.

Kwanza anaangalia kisa kizima cha kutaka kuuawa Cloud na anagundua kuwa ni fitina tu, lakini ukweli ni kwamba bosi huyo hajafanya kitu chochote kibaya kwa wenzake ili alipiziwe kisasi, badala yake ni husuda tu.

Badala ya kumuua, anaamua kumlinda. Lakini akaangukia kwenye penzi na mwanaume huyo.

Cloud mwenyewe akawa hajui chochote. Mara ya kwanza alipomuona alimpenda na wakawa wapenzi. Kwa maana hiyo ilikuwa ni rahisi tu kwa jini Irene kummaliza mtu wake.

Kazi ya pili ya Irene ilikuwa ni kumuonya wa msaidizi wa bosi Cloud kuacha kutaka kumdhuru mwenzake, la sivyo atakiona cha moto.

Irene anamtokea msaidizi wa bosi na kumuonya, lakini anapoleta dharau, jini linajipambanua kuwa hakuwa mwanamke halisi kama anavyodhani, hivyo jamaa huyo anaingia woga na kwenda kumwomba msamaha Cloud kwa yote aliyomtendea.

Cloud anashangaa msamaha huo na hajui chanzo chake ni nini, kumbe ni mpenzi aliyenaye ambaye yeye anadhani ni binadamu wa kawaida.

Tatizo linakuja kwenye kuoana, kwani Irene anakataa na kumwambia kuwa hawezi kuolewa na binadamu kwa sababu yeye ni mtu wa kawaida.

Majibu hayo kwake Cloud anayaona kama ni ya dhihaka na hayana ukweli wowote ule.

Ili kumkomoa, anatafuta mpenzi mwingine kwa ajili ya kumuoa ili aachane na Irene ambaye inaonekana hataki kuolewa.

Lakini kila wanapofika nyumbani, wanamkuta Irene ndani akiwa ameingia humo bila kufungua mlango. Hilo linamtisha Cloud na kuanza kukumbuka yale ambayo amekuwa akiyazungumza mara kwa mara.

Hali hii ilianza kumkosesha raha Cloud na kuanza kugombana na mpenzi wake Irene.

Siku iksiyo na jina wakiwa chumbani, Irene alitoa ya moyoni na kumwambia mambo yote kuwa yeye ni binadamu wa kawaida ila ni jini aliyekuja duniani kumuua. Alitumwa na msaidizi wake ofisini, lakini badala ya kufanya hivyo akaangukia kwenye penzi lake, na amefanya kazi kubwa kumsaidia kiasi kwamba hatari ya kuuawa imeisha kabisa.

Akamwambia muda wake wa kukaa duniani imeisha na sasa anaondoka, hivyo anampa ruhusa kuoa.

Awali Cloud alikuwa ni utani, lakini ghafla Irene alitoweka. Hakumuona tena. Baada ya miaka kadhaa Cloud alimvisha pete mchumba wake mpya. Akiwa kwenye harakati hizo, jini Irene alijitokeza ghafla. Alishtuka na kudhani atharibu sherehe. Lakini jini alipiga makofi kukubaliana na alichokifanya, akatoweka tena.



# SAFARI YA NIGERIA

## CARD B WASIWASI TELE KWA MUMEWE

RAPA mwenye makeke mengi, Cardi B, amewaomba mashabiki wake kufanya kila jitihada kumshwishi mume wake Offset, kukubali mpango wake wa kuhamia nchini Nigeria.

Hivi karibuni msanii huyo ameibua mjadala mkali baada ya kueleza kuwa ana mpango wa kuhama Marekani na kwenda kuishi Bara la Afrika ambako anasema ni sehemu yenye furaha kwake.

Hata hivyo, Cardi B hawezi kuondoka peke yake bila kuungana na mume wake Offset.

Mwanamuziki huyo alikwenda katika ukurasa wake wa Twitter siku ya Jumatatu na kuposti picha inayoonyesha akiwa na mume huyo ambaye alivaa vazi la kitamaduni la Kinigeria.

Katika picha hiyo aliandika ujumbe ambao aliwataka mashabiki wake kumsihi Offset, akubali kuhama pamoja naye.

"Mshawishini kuondoka na mimi," aliandika Card B.

Aliwataka mashabiki wake hasa kutoka Nigeria, kupasa sauti zao kwa kushiriki picha hiyo ili kumlainisha mume wake akubali kuungana naye katika makazi mapya.

Ujumbe huo uliitikiwa vilivyo kwa idadi kubwa ya watu kujitokeza kumuomba Offset akubali ombi la mke wake.

Wito wa kuamua kuhama Marekani aliutoa siku chache zilizolizopita, ambapo Cardi B baada ya Rais wa nchi hiyo Donald Trump, kuthibitisha kuuawa kwa Jenerali wa Jeshi wa Iran, Qassem Soleimani.

Tukio hilo limezidisha joto nchini humo baada ya raia kuwa na wasiwasi wa kuibuka kwa vita ya tatu ya dunia.

Cardi B ni mmoja wa watu wanaoamini kwamba kitendo cha Trump, kuamuru kuuawa kwa Soleimani, inaweka nchi hiyo katika hatari.




# Lil Wayne wanakusubiri Nigeria

IDADI ya wanamuziki wa Marekani wanaozuru Nigeria inazidi kuongezeka, sasa rapa Lil Wayne, ameelezea nia yake ya kwenda nchini humo.

Lil Wayne atakanyaga ardhi ya nchi hiyo miezi mitatu baada ya Card B kufanya hivyo na kupata mafanikio makubwa.

Mshindi huyo wa tuzo mbalimbali, alizungumza katika mahojiano kwamba sehemu ambayo anaipenda kwenda kuwa Nigeria.

"Sijawahi kufika Nigeria na ningependa kwenda na pia sijakwenda Misri, nafikiri huko kuna mawazo tofauti," amesema Wayne.



## Rob hukujua hafai au unajikosha tu!

Rob Kardashian, ameibua mjadala mpya baada ya kumwelezea mpenzi wake wa zamani Blac Chyna, kuwa ni hatari kwa malezi ya mtoto wao wa kike.

Kulingana na mtandao wa TMZ, Bob ambaye ni kaka wa Kim Kardashian, aliandika kisheria kwamba anataka kumlea binti yao Dream (3) katika malezi ya awali kutokana na mama yake hawezi kutoa malezi mazuri.

Amesema Chyna anazungukwa na watu wasiostahili akiwamo dada yake Khloe, na kwamba matumizi ya pombe kupita kiasi yanamfanya asikumbuke majukumu yake kama mama.


## 'The Legend of Inikpi,' hii hapa

MWIGIZAJI nyota kutoka Nollywood, Mercy Johnson, ametambulisha filamu yake mpya ya mwaka huu inayoitwa 'The Legend of Inikpi'.

Filamu hiyo inazungumzia tamaduni ya jamii ya Igala kwenye ufalme wa Bini, ambapo imechezewa katika nchi za Nigeria na Ghana.

Katika filamu hiyo mastaa mbalimbali wamecheza akiwamo Sam Dede, Odunlade Adekola, Saidi Balogun, Paul Obazele na wengine.





## Bierber kumbe afya yake mgogoro

NYOTA wa muziki wa Pop kutoka Marekani, Justin Bieber. Hatimaye amefichua hali yake ya kiafya na kueleza anasumbuliwa na ugonjwa unaojulikana kitaalamu kama Lyme.

Justin amewatangazia mamilioni wa mashabiki wake kwamba napambana na ugonjwa huo na kuondoa uvumi kuwa amedhoofika kutokana na matumizi ya dawa za kulevya.


"Wakati watu wengi wakiendelea kusema Justin Bieber anaonekana kama shiti, walishindwa kugundua nimegundulika hivi karibuni na ugonjwa wa Lyme, ambao unaathiri ngozi yangu, utendaji kazi ya ubongo, nishati, na afya kwa ujumla," aliandika kupitia akaunti yake ya Instagram.

## Rahama ulikwenda PSG kumwona Neymar?

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Rahama Sadau, anaonekana kupenda mpira wa miguu kiasi cha kufunga safari hadi Ufaransa kuwaangalia wachezaji nyota.

Rahama hivi karibuni alitembelea uwanja wa Paris St Germain (PSG) na akaposti picha ambayo alionekana akiwa ndani ya uwanja huo na kusema anahisi uwepo wa Neymar na Mbappe.

Mchezo wa mpira wa miguu ni moja ambayo watu wengi wanapenda sana katika sehemu mbalimbali za ulimwengu na wanatarajia kukutana na nyota wanaowapenda. Mwigizaji wa Nollywood, Rahama Sadau, hivi karibuni alipata nafasi ya kukutana na baadhi ya nyota anaowapenda zaidi ya mpira. Akiwa uwanjani hapo alitembezwa na katibu mkuu wa timu hiyo, Victoriano Melero, na ni wazi itakuwa ziara yake yenye msisimko katika maisha yake.



MAKALA

# Mdaiwa anaweza kufungwa asipolipa deni

Na Mwandishi Wetu



Ni kawaida watu kukopeshana fedha katika shughuli za kibinadamu za kila siku hasa zile za uzalishaji.

Ni kutokana na hili baadhi ya watu hujikuta wameingia katika mfarakano ambao hata hivyo unatatulika kisheria.

Kwa wale ambao madeni yao hutokana na taasisi za fedha, kama benki hawa huwa sio rahisi kwao kukwepa kutokana na utaratibu makini wa utoaji wa fedha wa taasisi hizo.

Tatizo kubwa la kutolipana na kuleteana dharau huhusisha wadeni binafsi yaani mtu na mtu. Ni katika madeni haya ya watu binafsi ambamo msemo maarufu wa deni halifungi husikika.

Ni kawaida kukuta mtu amekopeshwa na hataki kurejesha akijiamini kuwa deni halifungi. Yumkini wapambe nao husikika wakisema, asikutishe deni halimfungi mtu.

Kwa makala haya tutapata kujua ikiwa ni kweli deni linafunga au halifungi.

**KESI YA MADAI**

Kesi za madai ni zile kesi zote ambazo si za jinai. Kesi za madai hazihusishi kudaiana pesa tu kama wengi wanavyojua. Hata masuala ya talaka, kudai fidia, mikataba, madai ya vitu kama nyumba, magari na vitu vingine huingia katika kesi za madai.

Kwa hiyo tunapojiuliza swali la ikiwa deni linafunga au halifungi tunaongelea hivi vyote. Hata hivyo tutajielekeza zaidi katika kudaiana fedha.

**JE, INARUHUSIWA KUPELEKA MADAI POLISI ?**

Unayo haki ya kufungua shauri ikiwa kuna mtu unamdai, lakini kwa sharti kuwa shauri lifunguliwe pahala stahiki. Wapo ambao hupeleka kesi za namna hii polisi japo huko si mahali sahihi kwa kesi za namna hii.

Polisi hujitahidi kuzitafutia ufumbuzi ambapo wakati mwingine hufanikiwa na wakati mwingine hushindwa. Ukweli ni kuwa kisheria, polisi hawana ruhusa ya kushughulikia kesi za madai hasa hizi za kudaiana hela na hata mali.

Madhara utakayoyapata utakapomfungulia kesi mdai wako polisi ni pamoja na kupoteza muda bila kupata ulichokitaka. Hii ni kwa sababu mdaiwa atakapokataa kutoa ushirikiano wowote, polisi hawana la kufanya.

Hawawezi kumfunga kwa sababu hairuhusiwi. Hawawezi kumpeleka mahakamani kwa sababu hawaruhusiwi kupeleka kesi za madai mahakamani.

Kwa hiyo mdaiwa uliyempeleka polisi akiamua kukomaa hawana la kufanya, utakuwa umepoteza muda na gharama.

**Unayo haki ya kufungua shauri ikiwa kuna mtu unamdai, lakini kwa sharti kuwa shauri lifunguliwe pahala stahiki. Wapo ambao hupeleka kesi za namna hii polisi japo huko si mahali sahihi kwa kesi za namna hii. Polisi hujitahidi kuzitafutia ufumbuzi ambapo wakati mwingine hufanikiwa na wakati mwingine hushindwa.**

Basi ieleweke kuwa kesi za madai kama hizi hutakiwa kufunguliwa mahakamani.

Yaweza kufunguliwa mahakama yoyote kutegemea na kiwango cha fedha unachodai.

Waweza kufungua mahakama ya mwanzo, wilaya na hata mahakama kuu. Usipeleke kesi ya namna hii polisi labda kama unalenga kumtisha mdeni na si kupata haki.

**JE, DENI HALIFUNGI KISHERIA?**

Hapana, deni linafunga. Ikiwa utashtakiwa kwa kudaiwa fedha na hukumu ikatolewa kuwa unatakiwa kulipa hizo fedha basi unatakiwa uzilipe.

Ikiwa hauna basi itaangaliwa kama una mali kama nyumba, gari au mali yoyote ambayo inaweza kukamatwa ili kulipia deni. Ikiwa hauna vitu hivyo, mali nyingine yoyote inayoweza kufidia deni, basi itatakiwa ukamatwe ufungwe kwa ajili ya deni hilo.

Kifungu cha 44 (1) cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai, kinasema kuwa mdaiwa anaweza kukamatwa katika muda na siku yoyote, na haraka kufikishwa mahakamani na kuwa mahakama inaweza kutoa amri ya kuwekwa kizuizini/kufungwa. Kwa hiyo deni linafunga labda mdai asiamue kuchukua hatua.

**JE, UKIFUNGWA DENI LINAISHA?**

Hapana, ukifungwa deni haliishi. Kifungu cha 46 ( 2 ) cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai kinasema kuwa, mdaiwa aliyeondolewa katika kifungo kwa sababu yoyote ile, iwe kwa kumaliza muda, ugonjwa au vinginevyo hatahesabika kuwa ameondolewa katika deni kutokana na kuachiwa huko.

Hii ina maana unatumikia kifungo kikiisha deni linabaki palepale.

Kifungo hakifuti au kusimama badala ya deni isipokuwa ni adhabu ya ukorofi.

Ni kutokana na mtazamo huo wa sheria inalazimisha kutakiwa kulipa deni hata baada ya kutumikia kifungo. Ukishindwa mara nyingine tena kulipa mdai anayo haki ya kukurudisha tena mahakamani ambapo unaweza kufungwa tena. Msimamo wa sheria ni mpaka ulipe tu.

**KULIPIWA DENI UKIWA JELA**

Muda wowote mdaiwa akiwa jela anatumikia adhabu yake ya deni anaweza kuondolewa na kufutiwa adhabu hiyo iwapo kiwango cha deni analodaiwa kitalipwa. Mahakama iliyotoa amri ya kufungwa ndiyo itakayotoa amri ya kuachiwa baada ya deni kulipwa katika ukamilifu wake.

**KWA MSAADA WA MTANDAO**

# TGNP na ilani ya uchaguzi 2020

Na Sabato Kasika

UWIANO wa jinsia kwenye ngazi za maamuzi, ni moja ya mambo ambayo wadau na wanaharakati wamekuwa wakikazania ili kuwapo na usawa kati ya wanawake na wanaume katika uongozi.

Miongoni mwa wadau hao ni Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), ambao umeanzisha kampeni ukitaka kuona mwanamke haachwi nyuma katika kugombea au kuchagua uongozi, katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu wa 2020.

Kutokana na hilo, shirika hilo lisilo la kiserikali, limesambaza Ilani ya Uchaguzi ya Wanawake kwa vyama vya siasa nchini, ambavyo ni wadau wakuu wa uchaguzi huo ili wanachama wake wasome yaliyomo na kuyafanyia kazi.

Mkurugenzi Mtendaji wa mtandao huo, Lilian Liundi, anasema, wao hawako nyuma na watahakikisha mwanamke anapata nafasi katika uchaguzi huo ikiwa ni mikakati ya kutafuta uwiano katika uongozi.

"Tulishazindua Ilani ya Uchaguzi ya Wanawake na kuigawa kwa wadau vikiwamo vyama vya siasa na pia kuvitembelea na kusikiliza jinsi vinavyotekeleza masuala ya kijinsia," anasema Liundi.

Mbali na hilo, Mkurugenzi huyo anasema, wamefanya uchambuzi na mapitio ya sera na ilani za vyama hivyo kuangalia mapengo na kushauri kufanya marekebisho mapema kabla ya uchaguzi mkuu.

"Hiyo inatokana na ukweli kwamba kuna jambo la kufanyia kazi, ili kuwe na mazingira mazuri, ambayo yatamwezesha mwanamke kuwa na nafasi na kushiriki vizuri katika uchaguzi mkuu," anasema.

Anasema, vyama vya siasa vinatakiwa kutoa fursa kwa wanawake kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kwa vile wanawake wenye sifa za kuwa viongozi wapo, hivyo ni muhimu hilo likafanyiwa kazi.




Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi (wa tatu kushoto) na wenzake wakiwa na viongozi Chama cha ACT - Wazalendo baada ya kukabidhi Ilani ya Uchaguzi ya Wanawake kwa chama hicho. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**ILANI YA WANAWAKE**

Liundi anasema, ilani hiyo imendaliwa na TGNP kwa kushirikiana na Mtandao wa Wanawake na Katiba, imewashirikisha kwa kukusanya maoni kutoka makundi yote nchini hasa vijijini.

Anasema, asasi za kiraia zinazotetea haki na usawa wa kijinsia zaidi ya 60 zimeshiriki kikamilifu kuandika na kukamilisha ilani hiyo.

Septemba mwaka jana, ilani hiyo inayojumuisha sauti za wanawake kutoka makundi mbalimbali ilizinduliwa rasmi.

Anasema, baadaye Oktoba ikasambazwa kwa wadau vikiwamo vyama vya siasa lengo likiwa ni kuhakikisha ilani hiyo inakuwa na mchango mkubwa kwenye uchaguzi huo ujao.

"Sisi wanawake wapigakura tunatambua ni wadau muhimu kwenye shughuli zote za kisiasa na maendeleo ya jamii. Tunatambua na kudai haki za kushiriki katika uchaguzi kama wapigakura na wanaowania uongozi, walioteuliwa na kugombea hatimaye kushinda nafasi za uongozi kupitia uchaguzi," anaongeza kusema;

**YALIYOMO NDANI**

Liundi anasema, ilani hiyo imebeba masuala muhimu yanayohusu wanawake kwenye uchaguzi, na kwamba imewalenga wanawake, serikali, vyama vya siasa, wagombea nafasi za uongozi, vyombo vya habari na wapigakura.

Anasema ilani hiyo ni ya tano ikiwa na madai ya wanawake kama wadau na washiriki wakuu katika michakato mbalimbali ya uchaguzi. "Madai yaliyomo ndani ya ilani yanahusu masuala ya wanawake wote nchini Tanzania, hivyo ni muhimu wote kuungana bila kujali itikadi za kisiasa na badala yake wawe kitu kimoja," anasema.

Anasema, lengo kuu la ilani hiyo ni kutoa sauti za pamoja za wanawake na makundi mbalimbali yanayotetea haki za wanawake na watoto kuhusu ushiriki kamilifu wao katika mchakato mzima wa uchaguzi.

Mkurugenzi huyo anasema, pamoja na hayo, ni kuhakikisha ajenda yao inapewa kipaumbele, katika mipango ya serikali inayopewa ridhaa ya Watanzania kuongoza nchi.

Anasema ilani hiyo inayoongozwa na kauli mbiu isemayo, "Ajenda ya Mwanamke, Turufu ya Ushindi 2019/2020" inasisitiza kuwa hatima ya nchi hii iko mikononi mwa wanawake na wanaume.

"Wapigakura wana uwezo mkubwa wa kuleta mabadiliko makubwa na ya kimapinduzi, katika nchi yetu endapo tutaunganisha nguvu zao na kufanya wanawake kama wapigakura kukataa kuuza haki zao," anasema.

Anasema, lingine ni wanawake kukataa kurubuniwa na vyama, viongozi au watu wenye uchu wa madaraka na tabia ya kudhalilisha wapigakura wao na pia wapigakura wakatae kuunga mkono vyama au viongozi watarajiwa wanaokumbatia mfumo dume katika uchaguzi mkuu.

**JUHUDI ZA SERIKALI**

Serikali inasema, inaendelea kuyachukulia hatua mbalimbali masuala ya usawa wa kijinsia, ili kuhakikisha inaongeza uwiano wa kijinsia kati ya wanaume na wanawake katika uongozi ili kufikia 50 kwa 50.

Inasema, bado kuna jitihada zaidi zinatakiwa kufanyika, ili uwiano huo wa kijinsia uweze kufikia 50 kwa 50, na ndiyo maana inachukua hatua mbalimbali kwa ajili ya kufikia uwiano huo.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alikaririwa akisema serikali inachukua hatua mbalimbali kupitia sera ya jinsia ya mwaka 2000 na itifaki mbalimbali za kimataifa kuwainua wanawake.

Waziri Mkuu anataja baadhi ya hatua hizo kuwa ni kujenga zahanati kwa ajili ya kupunguza vifo vya wanawake na watoto wakati wanajifungua na kuimarisha elimu ya msingi na sekondari.

Mbali na hizo, anataja nyingine kuwa ni kampeni ya kumtua mama ndoo, ili apate muda wa kutosha kushiriki shughuli mbalimbali za maendeleo, huku serikali ikiendelea kufuatilia kwa karibu kwa ajili ya kufikia azima hiyo.



Baadhi ya wadau wakiwa na Ilani ya Uchaguzi ya Wanawake baada ya kumaliza kuizindua.

**MAKALA**

# MAAJABU SHULE YA AGAPE

## ●Wanafunzi saba, wote wamefaulu
## ●DC asema wamepewa funzo

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE ya Msingi Agape, inayochukua mchepuo wa Kingereza iliyojengwa katika kijiji cha Bukima, Kata ya Bukima Wilaya ya Musoma, imewashangaza wengi baada ya kufanya vizuri katika matokeo ya taifa ya darasa la saba wa mwaka jana.

Shule hiyo ambayo imewaacha watu kubaki wakijiuliza, inatokana na idadi ndogo ya wanafunzi wanaosoma lakini kila mmoja anaonekana kuwa na upeo wa hali ya juu kitaaluma.

Akizungumzia kwa undani kuhusu shule hiyo, Ofisa Elimu wa Kata ya Bukima, Gimasa Luyembe, anasema kutokana na matokeo hayo kiwango cha ufaulu kwa kata umepanda kutoka asilimia 54 hadi 60.

Anasema, kata yake ina shule za msingi sita, ambazo ni Majita A, Majita B, Butata A, Butata B, Mkapa na Agape.

Lakini Agape ndio inaongoza licha ya kuwa na wanafunzi saba waliomaliza darasa la saba mwaka jana.

Ufaulu haukuwa kwa darasa la saba pekee, kwani darasa la nne iliongoza kiwilaya baada ya wanafunzi wake kufanya vizuri.

"Kwa mfano katika mtihani wa darasa la nne mwaka 2018 kwenye kundi lao kiwilaya, Agape ilikuwa ya kwanza, na mtihani wa taifa wa darasa la saba mwaka 2019 imekuwa ya kwanza," anasema.

Anasema, wanafunzi wote saba wa shule hiyo wamechaguliwa kwenda sekondari ya vipaji maalumu za Musoma Technical, Songe Girls na Bwiru Boys na wengine wakichaguliwa kusoma Sekondari ya Kata ya Bukima.

"Katika kata yangu, wanafunzi 182 wamechaguliwa kwenda sekondari wakiwamo hao wa Agape, ambao kwa kweli wamekuwa ni chachu kwa kata na hata wilaya kwa ujumla," anasema.

**DC APATA FUNZO**

Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney, anasema, shule hiyo imeiweka wilaya yake katika ramani, na kwamba ipo haja kwa shule nyingine kujifunza mbinu zinazotumiwa na Agape, ili kuongeza ufaulu.

"Sisi kama serikali, tutaendelea kushirikiana na shule hii ambayo kwa kweli imetutoa kimasomaso, kutokana na matokeo mazuri na ninaamini kuna jambo la kujifunza kutoka katika shule hiyo," anasema Dk. Annay.

Dk. Anney anasema, shule hiyo ipo eneo la Majita, ambalo zamani lilikuwa linatoa wasomi wengi wa Mkoa wa Mara, lakini baadaye hali ikabadilika na sasa imeanza kurejea upya, hivyo ni muhimu kuunga mkono juhudi hizo.

"Shule zetu za serikali hatuna budi kujifunza jambo kutoka Agape na kulifanyia kazi ili kuongeza ufaulu katika shule zetu, kwani nayo iko vijijini ndani ndani, lakini wanafunzi wake wanafanya vizuri," anasema.

Anasema, kwa njia hiyo, kiwango cha elimu kinaweza kuendelea kupanda kwenye eneo lote la Majita, ambalo ni miongoni mwa maeneo yaliyotoa wasomi wa fani mbalimbali.

"Kwa ujumla ni kwamba nimevutiwa na maendeleo ya shule hii ambayo mwaka jana ndio amekuwa na wanafunzi waliohitimu darasa la saba na wakafanya vizuri na kuipaisha wilaya yetu," anasema.



Uwekaji wa jiwe la msingi wa jengo la Tehama la shule hiyo uliofanywa na Prof. Sospeter Muhongo (kushoto). Wengine kulia ni mmiliki wa shule hiyo, Andrea Kayora na Diwani wa Kata ya Bukima, January Simula.



Mmiliki wa Shule ya Agape, Andrea Kayora akiwa ofisini kwake.

**NINI SIRI YA MAFANIKIO?**

Andrea Kayora ambaye ni mmiliki wa shule hiyo, anasema aliianzisha mwaka 2003, kwa kujenga chumba kimoja cha darasa akiwa na wanafunzi saba wa darasa la kwanza na walimu wawili.

Kayora anasema, kadri miaka ilivyokuwa inakwenda, ndivyo alivyokuwa akiongeza vyumba vingine vya madarasa na hatimaye mwaka 2017, shule ilisajiliwa na serikali.

"Bahati nzuri ni kwamba mwaka jana kwa mara ya kwanza, darasa la saba walifanya mtihani wa taifa, na shule yetu imekuwa ya kwanza kiwalaya kwa ufaulu wa madaraja ya juu," anasema Kayora.

Anasema, mwamko wa jamii kwenye elimu umeanza kuonekana, kwani shule hiyo ina wanafunzi 125, vyumba saba vya madarasa, walimu kumi na waangalizi wawili wa wanafunzi.

"Shule yetu imeongeza hamasa katika elimu katika Kata ya Bukima na Wilaya ya Musoma kwa ujumla ingawa bado kuna changamoto kadhaa, ambazo tunaendelea kukabiliana nazo," anasema.

Kayora ambaye kitaaluma ni mtawala, anasema hali ngumu ya uchumi inasababisha ujenzi wa miundombinu ya shule kufanyika taratibu, na kwamba anaamini atafika alikokusudia katika kuinua elimu vijijini.

"Baadhi ya malengo yangu ni shule kuwa na wanafunzi 175, idadi ambayo anaamini inatosha na pia ninatamani kuwa na sekondari, chuo cha ufundi stadi na ikiwezekana hata Chuo Kikuu cha Musoma," anasema.

**HISTORIA**

Kayora alizaliwa mwaka 1987 katika Kijiji cha Bukima na alihitimu elimu ya msingi mwaka 2001, katika Shule ya Msingi Majita na kisha kujiunga na Sekondari ya Adrian iliyopo Mzumbe mkoani Morogoro.

Kayora anasema, wakati akiwa kidato cha pili katika sekondari hiyo, kufanya ziara ta mafunzo nchi Ujerumani na kujifunza mengi yaliyomfanya awe na wazo la kuanzisha shule ya Kiingereza vijijini.

"Mwaka 2005 nilihitimu kidato cha nne na kujiunga na Sekondari ya Umbwe mkoani Kilimanjaro na kuhitimu kidato cha sita mwaka 2008 na kwenda Chuo Kikuu cha Dodoma," anasema.

Anasema, akiwa chuoni hapo, mwaka 2010, alifanya mafunzo ya kazi bungeni kwenye kitengo cha utawala na kujifunza mambo mbalimbali yanayohusu sekta hiyo, ambayo imemfanya amiliki shule.

"Mwaka 2011 nilihitimu Shahada ya Biashara Raslimali Watu, Bcom (HRM), nikarudi nyumbani kijijini Bukima kutimiza ndoto yangu ya kutoa mchango, katika elimu," anasema.

Anasema, alianza kujitolea kufundisha katika Sekondari ya Kata ya Bukima na kwa muda mfupi aligundua, wanafunzi wengi wa kidato cha kwanza na cha pili waliihofia lugha ya Kiingereza.

"Posho niliokuwa ninalipwa na Sekondari ya Bukima niliiwekeza katika Vicoba na baadaye nikakopa Sh. milioni tatu na kununua eneo la kujenga shule huku nikiendelea na kufanya mipango ya kutimiza lengo langu," anasema.



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Agape. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 28 00)



**Dondoo: Kulia**

1. Daraja fulani la watu
7. Mahabusu
8. Luanda ni mji mkuu
9. Mbolea
12. Kuwa madhubuti
14. Ekari
15. Rais mweusi wa kwanza Afrika ya Kusini
16. mojawapo ya wilaya Mbeya
18. begi
21. Nabii wa Mungu
22. Fahamu
23. Kuwa wa awali
26. rai za watu
27. Mto wa nne kwa urefu Afrika
28. Mirungi

**Dondoo: Chini**

1. Tia maanani, heshimu
2. Weka mdomoni na tafuna
3. Omba ruhusa ya kuondoka
4. Sehemu ya kitu, fungu
5. Jimbo jamhuri ya Dominiki
6. Chora chini
10. Hupumua kwa mapezi
11. Chombo cha bati cha kutilia vitu
13. Rudisha
17. Dumazwa
19. Madini
20. Awali
24. Kinyume cha ndani
25. Kataa kutii sheria za nchi

**Jibu toleo lililopita**

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| I | S | H | A | R | A | | K | A | M | U | S | I |
| N | | I | | | | | | | A | | A | |
| D | H | A | M | I | R | A | | A | T | I | B | U |
| O | | R | | M | | | M | | A | | A | |
| N | Y | I | M | B | O | | K | A | T | I | B | U |
| E | | | N | A | M | B | A | | I | | U | |
| S | | | Y | | B | | T | O | Z | O | | G |
| I | | T | A | B | O | R | A | | O | | | H |
| A | | | M | A | L | A | B | A | | U | M | A |
| | | K | A | P | E | R | A | | Z | | | R |
| M | T | U | | A | Z | U | | T | A | N | G | A |
| B | | K | | | A | A | L | A | M | | | M |
| A | J | U | Z | A | | | | A | U | N | I | A |

# Ajali ya ndege yapunguza joto mauaji ya Jen. Qasem Soleiman

MVUTANO wa mataifa ya Marekani na Iran kuhusu kuuawa kwa Jenerali Qasem Soleiman, unaanza kupoa taratibu. Hata hivyo kumeibuka na mzozo mwingine katika sura tofauti ambao unaendeleza uhasama kati ya nchi hizo.

Soleimani, ambaye aliongoza vikosi vya Qudsi vinavyoungwa mkono na Iran, aliuawa usiku wa Januari 3 wakati akitoka uwanja wa ndege wa Baghdad, nchini Iraq katika msafara wa magari.

Kifo chake kilifuatia na ulipizaji kisasi wa Iran, baada ya kurusha makombora 13 katika kambi mbili za Marekani zilizopo nchini humo.

Hata hivyo, wakati Iran inatekeleza hasira zake kwa kurusha makombora hayo, wakati huo huo ndege ya abiria ya Ukraine, ilianguka muda mfupi baada ya kupaa kutoka uwanja wa ndege wa Tehran.

Matukio hayo mawili yaliifanya dunia kubaki na mkanganyiko, kama macho yaelekezwe katika tishio la vita kati ya Marekani na Iran, au kuangazia ajali ya ndege iliyoangamiza maisha ya watu wote 176.

Hata hivyo, ajali hiyo imeonekana kuleta sura mpya katika mzozo huo, imeonekana kupunguza makali ya mzozo huo kiasi ambacho kila mmoja sasa amesahau kwa muda kifo cha Jenerali Soleimani.

Sasa dunia inataka kujua ajali ya ndege hiyo imesababishwa na nini? Huku baadhi ya mataifa ya Ulaya yakifanikiwa kubadilisha hali ya hewa kwa kutoa ripoti kwamba kuwa kombora la Iran lilidungua ndege hiyo kimakosa.

Viongozi wa Canada na Uingereza huku wakijaribu kukwepa kuilaumu Iran, wanataka uchunguzi wa kina ufanyike kubaini chanzo halisi kilichosababisha ajali hiyo.

Ukraine awali imekuwa na msimamo wa wastani ikisema inachunguza endapo ndege yake iliangushwa na kombora au la, wakati huo huo ilionya suala hilo lisichukuliwe kwa dhana ya pekee.

Katika uchunguzi uliofanywa na nchi hizo, ulibaini kuanguka kwa ndege hiyo kulitokea saa chache baada ya Iran kushambulia kambi za kijeshi za Marekani nchini Iraq kwa makombora ya masafa marefu.

Vyombo vya habari vya Marekani, vinaashiria ndege hiyo ilidhani kuwa ndege ya kivita ya Marekani wakati Iran ilipokuwa ikijiandaa kujibu mashambulio la kulipa kisasi.

Kituo cha habari cha CBS imevinukuu vyanzo vya kijasusi vya Marekani vinavyodai kuwa picha



Jenerali Qasem Soleiman.

za satelaiti zinaonyesha mwanga wa makombora mawili ambao ulifuatiwa na mwanga wa mlipuko.

Kituo cha habari cha CBS kimevinukuu vyanzo vya kijasusi vya Marekani, vinavyodai kuwa picha za satelaiti zinaonyesha mwanga wa makombora mawili ambao ulifuatiwa na mwanga wa mlipuko.

Kanda ya video iliyopatikana na New York Times ilionyesha jinsi makombora yalivyokuwa yakipita katika anga la Tehran na baadaye kulipuka ilipokutana na ndege.

Karibu sekunde 10 baadaye mlipuko mkubwa ulisikika ardhini. Ndege iliyoshika moto, inaendelea kupaa.

Rais wa Marekani, Donald Trump, juzi alisema kwa tahadhari kubwa kwamba ana shaka juu ya kuanguka kwa ndege hiyo.

"Inawezekana kuna mtu amefanya kosa kubwa." Alisema Trump.

Iran imetangaza kutokabidhi kisanduku cheusi cha kuhifadhi taarifa za ndege kwa kampuni ya ndege ya Boeing au serikali ya Marekani kwa ajili ya uchunguzi.

Hatua hiyo inatokana na mzozo uliokomaa baina ya Marekani na Iran, hasa baada ya Trump kuagiza shambulio la anga lililomuua Jenerali wa Iran Qasem Soleimani Januari 3.

Chini ya sheria za kimataifa za usafiri wa anga, Iran ina haki ya kuongoza uchunguzi wa ajali hiyo, lakini kawaida huwa kampuni iliyotengeneza ndege pia hushirikishwa kwa karibu.

Ndege hiyo ni Boeing 737-800 ambayo imetengenezwa Marekani, nchi ambayo ni hasimu wa Iran.

CBS na Newsweek waliripoti kuwa maofisa wa ujasusi wa Marekani na Iraq wana hakika kuwa ndege hiyo iliangushwa na makombora ya Iran.

CBS wamechapisha taarifa inayodai kuwa mitambo ya rada ya Marekani, ilibaini makombora mawili yakirushwa muda mfupi kabla ya ndege hiyo kulipuka.

Kwa upande wa Newsweek wamewanukuu maofisa wa Marekani na Iraq ambao wanaamini ndege hiyo ilidunguliwa na makombora ya Kirusi aina ya Tor M-1 ambayo Nato huyaita Gauntlet.

Maofisa wawili kutoka makao makuu ya jeshi la Marekani wameithibitishia Newsweek kuwa shambulio hilo lilikuwa la bahati mbaya.

**IRANI IMESEMA NINI?**

Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga wa Iran, Ali Abedzadeh, amesema, "ndege hiyo ambayo awali ilikuwa ikielekea magharibi baada ya kupaa ilikata kona kulia kutokana na hitilafu ya kiufundi na ilikuwa ikirejea uwanja wa ndege pindi ilipoanguka."

Abedzadeh ameongeza kuwa mashuhuda waliona ndege hiyo "ikiwaka moto" kabla ya kuanguka na kuwa marubani hawakutoa taarifa yoyote ya dharura kabla ya kujaribu kurudi uwanja wa ndege wa Imam Khomeini.

"Ndege kadhaa za ndani na nje zilikuwa zikipaa katika anga la Iran katika usawa wa futi 8,000 kama ilivyokuwa kwa ndege ya Ukraine. Hivyo suala la kupigwa na makombora haliwezi kuwa na ukweli wowote," ameongeza.

Ofisa huyo amedai kuwa taarifa za awali za uchunguzi zimeshapelekwa Ukraine na Marekani, ambapo ndipo makao makuu ya Boeing.



Mabaki ya ndege ya Ukraine iliyoanguka nchini Iran. **PICHA MTANDAO**

HABARI KIMATAIFA

# Mauaji ya Qasem Soleimani habari njema kwa IS

**BAGHDAD, Iraq**

HATUA ya Rais wa Marekani, Donald Trump, kuamuru kuuawa kwa Jenerali Qasem Soleimani, ambaye alikuwa mkuu wa vikosi vya Qudsi vinavyoungwa mkono na Iran, imeonekana kuleta furaha kwa kundi la Islamic State (IS) nchini Iraq.

Iran na vikosi ambavyo inaviunga mkono nchini Iraq wameapa kulipiza kisasi kwa mauaji ya Qasem Soleimani, yaliyosababishwa na bomu lililorushwa na ndege isiyokuwa na rubani ya Marekani.

Bomu hilo lililenga gari la Soleimani wakati linaondoka uwanja wa ndege wa Baghdad Ijumaa iliyopita.

Na pia hiyo ni hatua itakayofurahiwa na kundi la Islamic State ambalo litafanikiwa kujiimarisha tena kwa haraka baada ya utawala wake kuangushwa.

Pia ni habari njema kwa wenye msimamo mkali kwamba Bunge la Iraq lilipitisha muswada unaotaka raia wa Marekani kuondoka mara moja kote nchini humo.

Chimbuko la kundi la IS ni kundi la al-Qaeda nchini Iraq lililosambaratika na limekuwa imara kwa miaka mingi.

Operesheni kubwa ya kijeshi mwaka 2016 na 2017, ilihitajika ili kumaliza utawala wa kundi la IS nchini Iraq na Syria.

Wapiganaji wengi wa Jihadi waliishia kufa ama kuwa wafungwa, lakini hilo halikufanikiwa kusambaratisha kabisa kundi hilo.

Kundi la IS bado lipo imara katika maeneo ya Iraq na Syria ambako limesababisha uvamizi, ubadhirifu wa fedha na vifo kwa wengi.

Nchi ya Iraq ina jeshi na vikosi vya polisi bora waliopewa mafunzo na Marekani na washirika wa Ulaya waliojiunga katika vita dhidi ya IS.

Tangu mauaji ya Soleimani, Marekani imesitisha mafunzo yake pamoja na operesheni zake ikiwa ni pamoja na Denmark na Ujerumani.

Ujerumani inaondoa wanajeshi wake waliokuwa wanatoa mafunzo nchini Jordan na Kuwait.

Vikosi vya Iraq ndivyo vinakuwa katika hatari zaidi wakati wa operesheni ya ardhini dhidi ya IS.

Lakini pamoja na mafunzo, pia vimekuwa vikitegemea usafiri kutoka kwa vikosi vya Marekani ambavyo kwa sasa vinanyemelea ngome yao.

Wanamgambo wa IS wana jambo la kusherehekea. Wakati Trump ameamua kumuua Soleimani; huo ulikuwa ushindi mkubwa kwao baada ya Marekani kumuua mmoja ya adui zake.

Mwaka 2014, wanamgambo wa Jihadi walianza kufanya mashambulizi na kutwaa maeneo muhimu ya Iraq ikiwamo mji wa pili kwa ukubwa wa Mosul.

Ayatollah Ali al-Sistani, kiongozi wa kidini wa Kishia wa Iraq, alitoa wito wa kujihami kukabiliana na Wasunni wenye msimamo mkali.

Na maelfu ya vijana Wakishia wakajitokeza na kujitolea na kwa ushirikiano na Soleimani na kikosi chake cha Qudsi, walikuwa sehemu ya mabadiliko makubwa katika vikosi vya jeshi. Wanajeshi hao walikuwa wenye nguvu na uwezo mkubwa wa kukabiliana na IS.

Kwa sasa, makundi yenye kuungwa mkono na Iran yamejumuishwa kwenye Jeshi la Iraq chini ya muungano unaojulikana kama Popular Mobilisation.

Viongozi wa vikosi hivyo wamekuwa wamepata madaraka makubwa ya kisiasa.

*BBC*



Moshi wa vumbi ukionekana umetanda angani baada ya Mlima Popocatepetl kulipuka volcano. Mlima huo upo katika mji wa Puebla, katikati ya Mexico. **(PICHA: AFP)**

## Iran yakana kutungua ndege ya Ukraine

**TEHRAN, Iran**

IRAN kwa mara nyingine imekana madai kuwa makombora yake yaliidungua ndege ya abiria ya Ukraine karibu na mji mkuu wa nchi hiyo, Tehran Jumatano.

Mkuu wa mamlaka ya anga amesema ana 'uhakika' kuwa ndege hiyo haikushambuliwa na kombora.

Mkuu huyo alikuwa akijibu madai yaliyotolewa na viongozi wa nchi za Magharibi kuwa ndege hiyo ilidunguliwa na makombora ya Iran kimakosa.

Ushahidi unaashiria kuwa kombora la Iran lilidungua ndege ya abiria ya Ukraine iliyoanguka karibu na Tehran, kimakosa, viongozi wa magharibi wanasema.

Viongozi wa Canada na Uingereza wanataka uchunguzi wa kina ufanyike kubaini chanzo halisi kilichosababisha, ajali iliyowaua watu wote 176 waliokuwa ndani ya ndege hiyo.

Ukraine awali ilisema kuwa inachunguza endapo ndege yake iliangushwa na kombora, jambo ambalo mamlaka za Iran zilikanusha vikali.

Kuanguka kwa ndege hiyo kulitokea saa chache baada ya Iran kushambulia kambi za kijeshi za Marekani nchini Iraq kwa makombora ya masafa marefu.

Ndege hiyo ni Boeing 737-800 ambayo imetengenezwa Marekani, nchi ambayo ni hasimu wa Marekani.

CBS na Newsweek waliripoti kuwa maafisa wa ujasusi wa Marekani na Iraq wana hakika kuwa ndege hiyo iliangushwa na makombora ya Iran.

CBS wamechapisha taarifa inayodai kuwa mitambo ya rada ya Marekani ilibaini makombora mawili yakirushwa muda mfupi kabla ya ndege hiyo kulipuka.

Kwa upande wa Newsweek wamewanukuu maofisa wa Marekani na Iraq ambao wanaamini ndege hiyo ilidunguliwa na makombora ya Kirusi aina ya Tor M-1 ambayo Nato huyaita Gauntlet.

# Wauza majeneza wafukuzwa hospitalini

**LUSAKA, Zambia**

WAFANYABIASHARA wa kuuza majeneza wamepewa muda hadi Machi mwaka huu, kuondoa bidhaa zao karibu na hospitali moja iliyopo mjini Lusaka, nchini Zimbabwe, kutokana na kuwasababishia wagonjwa msongo wa mawazo.

Kulingana na gazeti la Dail Mail, limemnukuu Meya wa Mji wa Lusaka Miles Sampa, akisema kwamba wauza majeneza watahamishiwa maeneo ya makaburini iwapo hawataondoka.

Wafanyabiashara hao walikuwa wamefungua maduka yao nje ya Hospitali ya Chuo Kikuu, ambapo kuna chumba cha kuhifadhi maiti.

Inasemekana kwamba wagonjwa na jamaa zao waliwasilisha malalamishi yao katika mamlaka ya eneo, na kusababisha kuchukuliwa kwa hatua hiyo.

Meya Sampa alisema wauza majeneza hao walikuwa wanawapa wagonjwa msongo wa mawazo, na kufanya iwe vigumu kwao kupata nafuu.

Meya huyo pia amesema kwamba wameombwa kutafuta eneo mbadala la kuuza bidhaa zao hizo au wahamishwe hadi maeneo ya makaburini kuendeleza kazi zao.

Kwa kipindi kirefu biashara hiyo imekuwa kama mkombozi kwa vijana wengi kupata kipato, na pia kuwekwa kwa majeneza hayo hospitalini, kulionekana kama eneo sahihi la kuendesha biashara hiyo.

Biashara hiyo ilionekana kuhudumia zaidi wale wanaotoka maeneo ya mbali.

Wafanyabiashara hao wamekuwa wakitoa huduma zengine kama kutayarisha mwili na kuusafirisha. Huduma yao ilionekana kupunguza mzigo kwa waombolezaji ambao mara nyingi huwa katika hali ya kukosa ujasiri wa kufanya shughuli za kumwandaa marehemu.

Hata hivyo, biashara hiyo imekuwa ikitekelezwa karibu sana na wadi za wagonjwa ambao wamelalamika kwamba tukio hilo huwakosesha imani ya kupona, hasa pale waombelezaji wanapojitokeza nyakati za mchana na husababisha wagonjwa kufikiria zaidi kuhusu kifo badala ya uponaji.

Wakazi wanaamini kwamba majeneza hayastahili kuuzwa kwenye hospitali hiyo, kwa sababu hilo ni eneo linalostahili kuwapa wagonjwa moyo na utulivu wa akili badala ya kuwatia hofu.

*BBC*

# HADITHI

# Jumba Jekundu-35

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina.

Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

MLANGO wa gari ulifunguka. Edina aliteremka ndani ya gari kwa madaha. Baadhi ya kinadada na kinamama waliokuwa wakipita hapo walishindwa kuendelea na safari zao kwa kumtazama.

Alionekana ni tofauti kabisa nao. Nadhani walikuwa wakijiuliza, msichana mzuri na mrembo kama huyo ametokea wapi.

Ni kama maajabu ya kumwona twiga akiwa mjini badala ya mbugani.

Dar es Salaam ikiwa imefurika wasichana warembo kupindukia, wengi wao wakiwa wameuongeza urembo wao wa asili maradufu kwa vipodozi lukuki vilivyofurika madukani, lakini si kwa msichana huyu Edina.

Uzuri wake ulikuwa ni asili, akiongeza na urembo wa kike ambao haujamfanya kubadilika kupita kiasi au kuchusha.

Ngozi yake maji ya kunde iliifanya imeremete na kushawishi kuigusa. Tabasamu lake pia ni jambo la kawaida katika uso wake, ambalo lingeweza kununuliwa kwa fedha tu iwapo mwenyewe angejali kujiunga na chuo kimojawapo cha usanii na kuhitimu. Hali kadhalika, ziada hii haikutokana na macho yake maangavu, pua yake iliyochongoka wala meno yake meupe yaliyojipanga kikamilifu kinywani mwake kama mistari miwili ya punje za mahindi kwenye kibunzi.

Wanaume na vijana waliokuwepo eneo hilo nao hawakuwa nyuma kwenye mshangao kwa malkia huyo alishuka ndani ya gari alilokuwa akiendesha mwenyewe.

Umbile la msichana huyo liliwafanya kuwa kama wamepigwa ganzi. Siku hiyo hakuweka dawa ya aina yoyote ile kwenye nywele na kuzidi kuzipa mvuto.

Siku hiyo alivaa mavazi yenye heshima, sketi ndefu iliyovuka magoti na blauzi nyepesi iliyokifanya kifua chake kitoe picha ya uhai wa matiti yake.

Nadhani alijua anakokwenda. Moja kwa moja alikwenda kumkumbatia Meze.

"Shemeji, habari za siku nyingi?" Yalikuwa ni maneno machache, lakini yakagonga kwenye vichwa vya wote wawili, Kadili na Meze.

Meze alijua kabisa maana na neno shemeji. Alitambua sasa Edina amewekа wazi nia yake ya kuwa na Kadili, maana si kwa kumwita shemeji hivi hivi tu.

Mshtuko ulimpata pia Kadili. Pamoja na kwamba dalili zote zinaonyesha kuwa Edina anaelekea kuwa mpenzi wake, lakini hakuna sehemu yoyote ambayo wametamkiana kuwa wanapendana kimapenzi.




Lakini neno 'shemeji' alilolitamka kwa Meze, linaashilia, huo ni mwisho ya yale yote ambayo alikuwa akiota, akiomba.

"Nadhani hakuna kipingamizi tena, leo hii nitamwambia kuwa nampenda na yeye atasema kilicho moyoni mwake, natumaini kuwa anasema ananipenda kwa sababu vitendo vyake vinaonyesha hivyo." Aliwaza Kadili.

Alimwita kijana mmoja na kumkabidhi noti ya Sh. 1,000 ikiwa pamoja na kumpa maelekezo ya kulinda gari iliyopaki hapo hadi watakaporejea.

"Mbona hujaniambia kuwa unakuja mama?" Kadili alianza kwa kumlaumu, kabla ya kufuatiwa kicheko chepesi kutoka kwa Edina.

"Nilitaka 'kukusapraizi', sikutaka kukwambia na kukusumbua kufanya maandalizi yasiyo ya lazima, au nimekosea baba."

"Hapana, maana nilitaka kukuchinjia kuku." Alijibu na wote watatu wakaangua kicheko.

Wakati huo, tayari walikuwa wanaongozana kwenda nyumbani kwa kina Kadili.

Edina alikuwa kati. Upande wake wa kushoto alikuwa Kadili na walikuwa wameshikana mikono.

Upande wake wa kulia alikuwa Meze. Mkono wa Edina ulikuwa begani kwake, hivyo kuleta picha nzuri, iliyowavutia wengi waliowaona na kupishana nao, lakini bila kujua pale mwenye mali ni nani, hali iliyowafanya wambea washindwe kubaini.

Safari hiyo ya watu watatu waliokuwa kivutio kikubwa usawahilini iliishia kwenye nyumba moja ndogo ya vyumba viwili na sebule.

Matofali ya nyumba hiyo ambayo yalikuwa hayajapigwa 'chupingi' mengine yalibadilika rangi na kuonekana meusi kutokana na kutokuwa katika matunzo mazuri, lakini pia kuloana na mvua.

Mabati kwenye nyumba hiyo yaligeuka rangi na kuwa meusi kwa kutu, huku baadhi ya misumari ilikiwa imeshang'oka, huku baadhi ya mabati yakiinuka na kurudi chini kwa kunesanesa kutokana na upepo, yakitoa sauti ya kubughuzi kwa walio ndani, nje na hata wapita njia.

Juu pia kuna mabati ambayo misumari yake ilikua imeng'oka kabisa, lakini yaliendelea kuwepo hapo badala ya kungoka kwa upepo kutokana na kukandamizwa na matairi ya gari makuukuu.

"Karibu ndani." Kadili alimkaribisha Edina kwa furaha, lakini kwa mbali ile aibu ya hali yake ya ufukara ilimsuta, kwani aliyemkaribisha alikuwa ni mwanamke aliyetoka kwenye familia ya kitajiri.

Si kwa kusimuliwa bali kwa kuona mwenyewe alipotekwa na kupelekwa huko kuteswa, chini ya usimamizi wa mama Edina ambaye kwa sasa ni marehemu.

**"Mbona hujaniambia kuwa unakuja mama?" Kadili alianza kwa kumlaumu, kabla ya kufuatiwa kicheko chepesi kutoka kwa Edina.**

"Ahsante." Alijibu kwa bashasha.

Alikaribishwa kukaa kwenye kiti ambacho miaka kumi kilifaa kuitwa kochi. Lilikuwa ni kocho kuukuu, ambalo sponji zake zilikuwa zimenyofoka na kilichoonekana zaidi ni mbao za chini.

Bila kufikiri mara mbili mbili, Edina alikaa kabla hata wenyeji wake hawajafanya hivyo.

Pamoja na mazingira yote hayo ambayo kwake yalionekana kama mbingu na ardhi ya ya kwao, Edina alionekana mwenye furaha zaidi kuliko hata wenyeji wake.

Zilipita dakika mbili hivi za makaribisho. Hali ya ukimya ikataka kuchukua nafasi yake.

"Edina, karibu, hapa ndiyo nyumbani kwetu." Edina sasa akakaribishwa rasmi.

"Nashukuru kwa kupafahamu na nashukuru kwa kufika pia, maana nilikuwa na hamu siku zote kufika hapa."

Kadili alionekana kutotulia sehemu moja. Alinyanyuka na kumuacha mgeni wake na rafiki yake Meze waliendelea kupiga stori za hapa na pale.

Baada ya dakika tatu kupita, Kadili aliingia sebuleni akiongozana na wanawake wawili. Mmoja ni mama wa makamo na mwingine ni msichana ambaye umri wake haukutofautiana sana na Edina.

"Mama, napenda kukutambulisha kwa rafiki yangu, anaitwa Edina na Edina, huyu ni mama yangu mzazi." Kadili alinyamaza kidogo akiwatazama kwa zamu mama yake pamoja na Edina.

Edina alisimama na kupiga magoti kwa heshima zote.

"Shikamoo mama."

"Marahaba mwanangu, hujambo?"

"Sijambo mama, leo nimeamua kuja kuwatembelea."

"Karibu mwanangu, hapa ni kwako, karibu muda wote ule unakaribishwa."

Mama Kadili alishangazwa kwa uzuri na urembo wa mwanamke huyo. Hakuona kasoro yoyote kwenye mwili, nywele na nguo za mwanamama huyo.

Manukato yake yaliifanya nyumba zima mle ndani kunukia kana kwamba wote mle walikuwa wamejipulizia manukato hayo, au nyumna ndiyo imepuliziwa.

"Mhh, ndiyo maana mwanangu aliamua kujitoa muhanga kufa na kupona kwa msichana huyu. Amepata tabu sana. Amevumilia tabu sana na amekuwa mvumilivu kwa kila kitu. Alikuwa sahihi, huyu ni malkia wa uzuri." alijisemea moyoni.

"Eliza, kutana na rafiki yangu anaitwa Edina, bibie, huyu anaitwa Eliza ni dada yangu binamu, mtoto wa mjomba wangu aliyezaliwa tumbo moja na mama yangu."

Edina alisimama na kumkumbatia Eliza.

"Hujambo mrembo." Edina alimsabahi akiwa amemkumbatia.

"Sijambo mrembo." Alijibu.

Walitazamana kwa sekunde kadhaa. Eliza alikiri kuwa Edina ni mrembo wa warembo na hapo alipojua ni kwa nini Kadili alikuwa hakubali hata chembe suala la kumuoa yeye kama wazazi walivyotaka na akawa anapiga chenga au kuchelewesha mpaka aone imeshindikana kabisa.

Kwa Edina kufika pale, alijua kabisa kuwa biashara yake ya kuoana na kaka yake binamu Kadili imekufa rasmi.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA /MASHAMBA

**Viwanja vinauzwa** Kibaha Misugusugu. Ukubwa ni mita 20 kwa 20 (400m2). Bei ni 2,000,000/- Milioni mbili tuu. (5,000/=1m2). Unaweza kulipa kwa awamu ndani ya miezi mine. Huduma zote zipo. Kwa mawasiliano: 0714 090009 / 0767 090008. Vimepimwa.

### MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MKOPO WA HARAKA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITD (EFL).** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumalizia tenda etc. Kwa maelezo zaidi piga 0758 112 332. Karibu EFL.


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**au piga simu: 0782253676**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No;9/2020

Ombi la JUMANNE OMARI MAKELELE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu OMARI SAID MAKELELE
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 11/02/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 09/01/2020.

115580902

### CHETI KIMEPOTEA



**SAYUNI P. MLIGO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0745-0040** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa Mwaka 2009 kupitia TEMBELA SEKONDARI.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kwenye kituo cha polisi kilicho karibu.

Taarifa ya polisi:
**CHA/BI/20/VOL/CLV/95.**

115580802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: CHAMWINO MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;2/2020
Ombi la ALLY SAIDI SADIKI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SAIDI SADIKI MALIAMACHO

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 22/01/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 09/01/2020.

115581002

### KADI YA GARI IMEPOTEA

HATIBU MHEMBERE MBWAMBO Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 211 CVF.

Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya Polisi:
MOR/MOR/
RB/28738/2020.

115581102


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# KANE AIPA PIGO SPURS, ENGLAND

**LONDON, England**

NAHODHA wa Timu ya Taifa ya England, Harry Kane atafanyiwa operesheni ya goti lake la kushoto na atakuwa nje ya dimba hadi Aprili mwaka huu, klabu yake ya Tottenham imetangaza.

Mshambuliaji huyo aliumia wakati wa mchezo wa mwaka mpya alipofunga bao dhidi ya Southampton ambalo lilikataliwa kwa kuonekana ameotea.

Spurs sasa imebainisha kwamba, Kane atakosa kipindi kikubwa cha nusu ya pili ya msimu wa Ligi Kuu England.

Kwa kikosi cha England, habari hizo zimekuwa pigo kubwa kwa kocha, Gareth Southgate na kwamba anamkosa wakati wa kujiandaa na michuano ya Euro 2020, na hatakuwapo kwenye mchezo wa kirafiki wa Machi dhidi ya Italia na Denmark.

Hata hivyo, kutokana na muda ambao umetajwa kurudi kwake dimbani, Kane ataweza kuwa fiti kuelekea mwishoni mwa msimu 2019-20.

Tottenham ilisema katika taarifa yake: "Baada ya madaktari kumfanyia uchunguzi kwa wiki iliyopita, tunaweza kuthibitisha kwamba, Harry Kane atafanyiwa upasuaji kwenye goti la mguu wake wa kushoto.

"Mshambuliaji huyu aliumia goti wakati wa mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Southampton wiki iliyopita."

## BAYERN YAFUNGUKA HATIMA YA SANE

**MUNICH, Ujerumani**

KOCHA wa Bayern Munich, Hansi Flick, ameomba kusajili Januari hii na klabu inafanyia kazi maombi yake, lakini Hasan Salihamidzic amethibitisha kwamba, Leroy Sane hatajiunga na timu hiyo mwezi huu.

Mkurugenzi wa michezo wa klabu hiyo, Salihamidzic ameviambia vyombo vya habari wakati huu Bayern ikijifua mjini Doha, nchini Qatar.

Amebainisha kwamba, Bayern wanafanyia kazi maombi ya Flick, ambaye amepewa jukumu la kukinoa kikosi hicho hadi mwishoni mwa msimu baada ya kufukuzwa kwa Niko Kovac Novemba mwaka jana.

Salihamidzic awali alisema kuhusu usajili wa Januari: "Sidhani kama kitatokea chochote."

Hata hivyo, katika mkutano wake na waandishi wa habari Alhamisi, Salihamidzic alisema: "Hansi Flick ameomba ufanyike usajili mwezi huu kwa ajili ya kuimarisha kikosi. Hansi na mimi tunawasiliana mara kwa mara.

"Tunaangalia uwezekano, lakini ni ngumu kuimarisha kikosi wakati wa dirsha dogo la usajili la Januari."

Hata hivyo, mchezaji wa kimataifa wa Ujerumani, Sane, ambaye kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na klabu hiyo kutoka kule Manchester City, hatakuwa nyota mpya wa kikosi hicho Januari hii.




## ALLEGRI ATAJWA KUTAKIWA UNITED

**MANCHESTER, England**

KOCHA Massimiliano Allegri ametajwa kwamba anajiandaa kupewa kazi katika kikosi cha Manchester United wakati wowote kuanzia sasa, kwa mujibu wa ESPN.

Kocha huyo amekuwa hana timu tangu aliopoondoka kwa miamba wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Juventus mwishoni mwa msimu wa 2018-19.


Hata hivyo, Allegri anaweza kurudi haraka kazini baada ya United kutajwa ikimwania kwa udi na uvumba.

Mtaliano huyo inaaminika kwamba yeye mwenyewe anapenda zaidi kwenda kuinoa United ambayo inachechemea kwenye Ligi Kuu England.

Massimiliano anataka kuchukua nafasi ya kocha, Ole Gunnar Solskjaer ambaye ameshindwa kufikia malengo ya klabu hiyo kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail.

Allegri pia amekuwa akivumishiwa kutakiwa na Bayern Munich na pia alikuwa anapewa nafasi ya kuchukua mikoba ya Arsenal kabla ya kupewa Mikel Arteta.

Hata hivyo, nafasi hiyo pale United inaonekana kuwa na ushindani mkubwa kwani, kocha wa zamani wa Tottenham, Mauricio Pochettino naye anatajwa kuhusishwa na nafasi hiyo.



## HABARI MICHEZO



# SIMEONE

## ASIFIA NYOTA WAKE KUING'OA BARCELONA

**JEDDAH, Saudi Aarabia**

DIEGO Simeone amekisifia kikosi chake cha Atletico Madrid kwa kufanikisha "jambo lililonekana kutowezekana" kwa kuifunga Barcelona kwenye hatua ya nusu fainali ya Kombe la Supercopa de Espanas.

Atletico iliifunga Barca mabao mawili ndani ya dakika tisa za mwisho na kuweza kuibuka na ushindi wa magoli 3-2 nchini Saudi Arabia, juzi Alhamisi.

Penalti ya Alvaro Morata na bao la Angel Correa liliwafanya Atletico kutinga fainali watakayokutana na wapinzani wao wa jiji moja, Real Madrid na ushindi huo ulionekana kuwa usiowezekana kwa kocha Simeone.

"Nafikiri tunatakiwa kuwa watulivu, kwamba tumefuzu kucheza fainali. Ni muhimu kwa mashabiki, ni muhimu kwa klabu, ni muhimu kwa wachezaji," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Ulikuwa mchezo mgumu dhidi ya timu bora duniani. Wao ni bora linapokuja suala la kumiliki mpira, na halafu kushambulia.

"Tulikuwa na wakati mgumu kipindi cha kwanza. Nafikiri kipindi cha pili kilikuwa tofauti, walionyesha ubora wao hadi tulipopota nafasi dakika ya 75, wakati ilipoonekana kuwa Atletico Madrid - wako bora zaidi.

"Tulikabiliana na wakati mgumu, ni kama jambo lililokuwa haliwezekani. Lakini tulikuwa na hisia kwamba tunaweza kusawazisha, na tunaweza kushinda, na hicho ndio kilichotokea."

Atletico itacheza fainali na Real Madrid hapa Jeddah Jumapili.

# Suarez amtetea Valverde kwa kipigo

**JEDDAH, Saudi Arabia**

LUIS Suarez amesema kwamba, kocha aliyekalia kuti kavu Barcelona, Ernesto Valverde sio wa kulaumiwa kwa timu hiyo kutolewa kwenye nusu fainali ya Kombe la Supercopa de Espana dhidi ya Atletico Madrid.

Barca walifungwa mabao 3-2 na Atletico kwenye nusu fainali ya Supercopa, kwa kuruhusu mabao mawili ya haraka dakika za mwisho hapa Saudi Arabia, juzi Alhamisi.

Mabao kutoka kwa Lionel Messi na Antoine Griezmann yalisawazisha lile la mapema la Koke alilofunga dakika ya 46 hadi Barca walipofungwa mabao mawili ndani ya dakika tisa za mwisho na kuipa ushindi Atletico inayokwenda kuvaana na Real Madrid.

Matokeo hayo yamezidi kuleta sintofahamu kuhusu majaliwa ya kocha, Valverde, lakini Suarez amemtetea kocha huyo mwenye umri wa miaka 55.

"(Valverde) sio wa kulaumiwa, makosa yalikuwa ya kwetu na sisi ndio tuliosababisha," alisema Suarez akiwaambia waandishi wa habari.

"Sijui kama kipigo hicho kitatusaidia sisi kukua, lakini kipigo hiki kinaonyesha tunatakiwa kujirekebisha mahali fulani.

"Inaonyesha kwamba, kuna makosa ambayo tunaweza kuyafanya na tukashindwa kabisa kuyasahihisha, lakini hili ni somo zuri kwetu."

# Arteta amhakikishia nafasi Xhaka

**LONDON, England**

MIKEL Arteta amemshawishi Granit Xhaka kubakia Arsenal baada ya kumwahidi kiungo huyo atafurahia tena soka lake.

Xhaka alionekana kupanga kuondoka Arsenal mwezi huu wa kipindi cha dirisha dogo la usajili, akiwa amehusishwa na kwenda kujiunga na Hertha Berlin.


Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uswisi alipokonywa unahodha na kupewa Pierre-Emerick Aubameyang baada ya mgogoro wake na mashabiki wa Arsenal wakati wa mchezo wa nyumbani dhidi ya Crystal Palace Oktoba mwaka jana.

Kiungo huyo wa zamani wa Borussia Monchengladbach, Xhaka aliripotiwa kufikia makubaliano na Hertha, lakini Arteta sasa anaamini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 atabakia Arsenal.

"Ujumbe wa kwanza kwake ulikuwa nataka kuelewa namna anavyojisikia na kwanini alikuwa akihisi hivyo," alisema Arteta, ambaye ameshinda mechi zake mbili kati ya nne tangu aanze kuwanoa washikabunduki hao, akiwaambia waandishi wa habari.

"Nilitaka yeye kunisikiliza mimi ushauri wangu, na kwamba nilikuwa tayari kumpa sapoti yoyote na pia kuishawishi klabu kumpa pia sapoti, kwa sababu nilifikiri yeye ni mchezaji mzuri kwetu na anaweza tena kufurahia soka lake hapa akiwa chini yangu.

"Nilijaribu kumshawishi kwa namna hiyo. Alifikiria kuhusu hilo, na alikuwa na majibu chanya na nikajua ameshabadili maamuzi yake."



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# CHELSEA YAJITOSA KUMWANIA LEMAR

●●●Lakini klabu yake ya Lyon yaweka wazi haiko tayari kumuuza winga huyo Januari...

**LONDON, England**

SIKU nyingine, muda mwingine wa kufahamu hatima ya Thomas Lemar.

Gazeti la The Guardian limeandika kuwa Chelsea imeweka wazi kuanza mchakato wa kuwania saini ya winga huyo wa Atletico Madrid ambaye pia anawindwa na klabu nyingine za Ligi Kuu England ambazo ni Tottenham na Arsenal.

Chelsea inaamini kuwa itafanikisha mchakato wa kupata huduma ya Lemar, huku taarifa zaidi zikiitaja klabu hiyo ya Stamford Bridge kukaribia kukamilisha mchakato wa kumnasa Mfaransa huyo ili kujiunga na kikosi hicho kinachonolewa na Frank Lampard.

Hata hivyo Chelsea inataka kumsajili kwa mkopo hadi mwishoni mwa msimu huu.

Winga huyo mwenye umri wa miaka 24 anaonekana 'kumvuruga' kocha Diego Simeone tangu alivyotua kwa dau la Euro milioni 72 akitokea Monaco mwaka 2018 kwa kushindwa kuonyesha kile kilichotarajiwa.

Mfaransa huyo anaonekana kuwa tayari kujiunga na klabu hiyo ya London Mashariki baada ya kushindwa kufunga katika mechi 21 alizoichezea Los Colchoneros msimu huu.

Katika kujiimarisha zaidi, The Blues pia inataka kumsajili straika wa Lyon, Moussa Dembele, ESPN imeandika, lakini huenda ikampoteza Wilfred Zaha baada ya Crystal Palace kumwitaji mshambuliaji huyo ambaye thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 80.

Imeelezwa kwamba The Blues wamewasilisha rasmi ofa ya Euro milioni 40 ili kumwania Dembele ambaye ana umri wa miaka 23 ili kurejesha makali katika kikosi chake.

Ingawa nyota huyo wa zamani wa kikosi cha vijana cha U-21 cha Ufaransa ameonyesha nia ya kurejea kucheza soka England, klabu hiyo ya Ufaransa imeweka wazi haina mpango wa kumuuza nyota huyo katika dirisha dogo la Januari, haswa kutokana na kuwakosa wachezaji wake muhimu, Memphis Depay na Jeff Reine-Adelaide, ambao ni majeruhi na watakaa nje hadi mwishoni mwa msimu huu.

Chelsea pia inatajwa huenda ikawauza nyota wake Olivier Giroud au Michy Batshuayi mwezi huu.

## KWA UFUPI

**FELLAINI KUREJEA LONDON**

KOCHA wa West Ham, David Moyes anataka kumsajili kiungo Mbelgiji Marouane Fellaini (32), kwa mara ya tatu kwa kumrejesha jijini London akitokea Shandong Luneng. ***(Sky Sports)***

**DEMBELE ANUKIA SPURS**

TOTTENHAM Spurs inajiandaa kuwania saini ya straika wa zamani wa Celtic, Moussa Dembele (23), kutoka Lyon baada ya kufahamu itamkosa mshambuliaji wake majeruhi, Harry Kane ambaye atarejea uwanjani Aprili mwaka huu. ***(Goal)***

**ERIKSEN AAMUA KUFUNGUKA**

MANCHESTER United imekubaliana na uamuzi wa kiungo wa Tottenham na Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen (27), kwamba anataka kwenda nje ya England na si kutua hapo Old Trafford. ***(Evening Standard)***

**SEMEDO KUONDOKA BARCA**

MABOSI wa Spurs wameweka wazi wanahitaji saini ya beki wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Ureno, Nelson Semedo, ambaye ana umri wa miaka 26. ***(Mirror)***

**BALE ARUDISHWA SOKONI**

REAL Madrid bado ina mpango wa kumuuza mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Wales, Gareth Bale (30), licha ya wakala wa nyota huyo kusema kuwa mchakato huo hauwezi kufanyika. ***(Telegraph)***

**DIALLO AKARIBIA CHELSEA**

STRAIKA wa FC Metz, Habib Diallo anawindwa na Chelsea, na klabu hiyo ya Stanford Bridge iko tayari kutoa ada ya pauni milioni 17 ili kumnasa nyota huyo raia wa Senegal ambaye ana umri wa miaka 24. ***(Star)***

**EMERY: EVERTON WALINIHITAJI**

KOCHA wa zamani wa Arsenal, Unai Emery, ameweka wazi kuwa alifanyiwa usaili wa saa tatu na Everton ambao baadaye waliamua kumpa kazi Carlo Ancelotti. ***(Mail)***

**COUTO ANUKIA ARSENAL**

ARSENAL imejiunga kwenye vita ya kuwania saini ya beki wa kulia, Yan Couto, mwenye umri wa miaka 17, na anaichezea klabu ya Coritiba ya nchini Brazil. ***(Globoesporte - via Metro)***

**BARCA, ARSENAL VITANI**

BARCELONA itapambana na Arsenal katika kuwania saini ya beki wa Timu ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 21 ya Ufaransa na RB Leipzig, Dayot Upamecano. ***(Express)***

**FERNANDES KIMEELEWEKA**

WEST Ham imekubali dili la kumsajili kwa mkopo wa miezi 18 kiungo wa Benfica na Timu ya Taifa ya Ureno, Gedson Fernandes (21), bila ya kuwapo kwa kipengele cha kumnunua hapo baadaye. ***(Mail)***

**LOOKMAN KUIKAMUA NEWCASTLE**

NEWCASTLE imetakiwa kulipa ada ya zaidi ya pauni milioni 22.5 kama atahitaji saini ya mshambuliaji wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya Vijana ya England (U-21), Ademola Lookman. ***(Northern Echo)***



HABARI MICHEZO

# KATWILA: KILICHOIUA YANGA NI HIKI HAPA

**Na Isaac Kijoti, ZANZIBAR**

KITENDO cha kuamini imemaliza mchezo na wachezaji wa Mtibwa Sugar kufuata maelekezo vema, ndicho kilichoisaidia kupata bao la 'usiku' la kusawazisha na hatimaye kushinda kwa changamoto ya mikwaju ya penalti dhidi ya Yanga juzi, kwa mujibu wa kocha Zuberi Katwila.

Katika mechi hiyo ya nusu fainali ya Kombe la Mapinduzi iliyopigwa Uwanja wa Amaan, Yanga ilipata bao la kuongoza katika dakika ya 36 kupitia kwa Deus Kaseke.

Bao hilo lilidumu hadi dakika ya 90 kabla ya Shomari Kibwana kusawazisha na hatimaye mikwaju ya penalti kuchukua hatua yake na Mtibwa Sugar kushinda kwa matuta 4-2, hivyo kutangulia fainali.

Akizungumza na Nipashe baada ya mechi hiyo, Kocha wa Mtibwa Sugar, Katwila, alisema wangeweza kumaliza mchezo huo mapema, lakini wachezaji wake walishindwa kutumia nafasi nyingi walizopata.

Katwila ambaye mwaka 2010 alitwaa kombe hilo wakati akiichezea Mtibwa, alisema alibaini makosa aliyokuwa akiyafanya Kibwana kabla ya kumuita na kumpa maelekezo ambayo aliyatekeleza.

"Niliwataka wachezaji kutulia na kuongeza umakini kwa dakika zote 90, na zaidi nilitoa maelekezo kwa Kibwana ambaye alikosa nafasi nyingi za kufunga na hatimaye akatekeleza kwa kutusawazishia," alisema.

Alisema kilichoigharimu Yanga zaidi ni kuamini wamemaliza mchezo na kutopambana kwa dakika zote 90.

Aidha, kuelekea mechi ya fainali Jumatatu ijayo, Katwila alisema kikosi chake kipo tayari kuvaana na timu yoyote iwe Azam au Simba.

"Unapoingia fainali utakuwa tayari kucheza na yeyote, kama ukiniuliza ni chague, basi nitakwambia nisikutane na yeyote," alisema.

Katika mechi hiyo ya juzi, Kipa wa Yanga, Ramadhani Kabwili alipangua penalti ya kiungo Abdulhalim Humud, hata hivyo, beki Kelvin Yondani aligongesha mwamba na kiungo Abdulaziz Makame akapaisha juu ya lango.

Wafungaji wa penalti za Mtibwa Sugar walikuwa ni Omary Sultan, Dickson Job, Jaffary Kibaya na Shomari Kibwana na zile za Yanga zilifungwa na Paul Godfrey 'Boxer' na kiungo Mapinduzi Balama.



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17, wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Dunia kwa vijana dhidi ya Burundi itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam. **PICHA: TFF**

# Taswa 'yawaamsha' wanachama wake

**Na Sabato Kasika**

KAMATI ya Utendaji ya Chama cha Waandishi wa Habari za Michezo nchini (TASWA), imewahimiza wanachama wake wenye nia ya kushiriki mkutano mkuu maalum wa chama hicho kuhakikisha wanathibitisha kwa maandishi ili kuhudhuria mkutano huo.

Katibu Mkuu Taswa, Amir Mhando, alisema jana hatua hiyo inatokana na mwitikio mdogo waliothibitisha kushiriki, hivyo kusababisha maandalizi mengine ya mkutano huo kushindwa kufanyika vizuri.

"Mwisho ya kuthibitisha kushiriki itakuwa Jumatatu Januari 13 mwaka huu, na mkutano mkuu sasa utafanyika Jumapili ya Januari 19, na hakutakuwa na muda wa ziada," alisema Mhando.

Aliongeza kuwa lengo la mkutano huo ni kujadili masuala mbalimbali ya chama, ambapo pia utapokea taarifa kutoka Kamati ya Marekebisho ya Katiba iliyoundwa na Baraza la Michezo la Taifa (BMT).

Alisema kwa mazingira hayo, ili mkutano ufanyike kwa ufanisi, ni vyema yeyote mwenye nia ya kushiriki athibitishe kwa maandishi akitaja jina lake na chombo na kutuma kwa email: taswatz@yahoo.com au mgosius@yahoo.com au machagift@gmail.com, ili taratibu nyingine ziendelee.

# Simba Queens yaendelea kung'ara

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Simba Queens imeendelea kufanya vizuri baada ya kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Mlandizi Queens katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani juzi.

Ushindi huo unaifanya Simba Queens inayofundishwa na kiungo wa zamani wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba, Mussa Hassan 'Mgosi' imefikisha pointi 17 na kukaa katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo yenye timu 12.

Katika mechi nyingine ya ligi hiyo iliyochezwa juzi, JKT Queens ilipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Yanga Princess na mabingwa hao watetezi wamefikisha pointi 16.

Matokeo hayo yanaifanya Yanga Princess inayonolewa na kiungo wa zamani wa Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), Edna Lema kubakia na pointi 12, huku kwenye msimamo wa ligi ikiwa kwenye nafasi ya nne.

"Mechi ilikuwa ngumu ya yenye upinzani, Yanga Princess imeimarika tofauti na ilivyokuwa msimu uliopita, ina wachezaji sita iliyowasajili kutoka katika timu yetu, hata hivyo tutajiimarisha licha ya wachezaji wengi wazuri kuwa tayari wameshasajiliwa na timu nyingine," Kocha wa JKT Queens, Ally Ally alisema.

Alliance Queens ya jijini Mwanza yenye pointi 19 ndiyo kinara wa ligi hiyo wakati Panama Queens ya mkoani Iringa inaburuza mkia ikiwa na pointi tatu mkononi.

Ligi hiyo inayodhaminiwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti, inatarajiwa kuendelea tena Jumamosi katika viwanja mbalimbali hapa nchini.

# JAMHURI YAJIVUNIA MAPINDUZI CUP

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA wa Jamhuri, Mustapha Hassan, amesema michuano ya Kombe la Mapinduzi imewapa mazoezi mazuri wachezaji wake katika kuelekea kwenye mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar.

Jamhuri ambayo inatokea kisiwani Pemba iliondolewa katika mashindano hayo yanayoendelea na Yanga kutoka jijini Dar es Salaam kwa kufungwa magoli 2-0.

Mustapha alisema licha ya kuondolewa mapema katika michuano hiyo, lakini mchezo huo umekipa kikosi chake kwa kuwapima nyota wake na timu yenye wachezaji wenye uzoefu wa kushiriki mashindano mbalimbali.

Kocha huyo alisema kuwa anaamini wataingia tofauti na wakiwa imara katika mechi zao zinazofuata za Ligi Kuu Zanzibar baada ya kumalizika kwa michuano hiyo.

"Ligi Kuu Zanzibar ina ushindani mkali hususani pale tunapokutana na timu za Kisiwa cha Unguja," alisema kocha huyo.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar, Jamhuri iko katika nafasi ya 10 kwenye ligi hiyo inayoshiriki klabu 16 na msimu huu ikitarajia kuteremsha timu sita.

# Michezo

Jumamosi Januari 11, 2020
Nipashe



## Chelsea yajitosa kumwania Lemar

HABARI UK 30




Golikipa Mbrazili wa Barcelona, Neto akimkwatua winga wa Atletico Madrid, Victro Perez 'Vitolo' (kulia), katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya Kombe la Mfalme nchini Hispania iliyochezwa juzi usiku. Barca ililala mabao 3-2. **PICHA: MTANDAO**

# MBELGIJI WA YANGA KICHEKO, Z'BAR VILIO

## ●●●Mashabiki walia kuikosa dabi, kocha huyo mpya aonyesha kukunwa na pasi za kasi pamoja na...

**Na Isaac Kijoti, ZANZIBAR**

AKIISHUHUDIA jukwaani kwa mara ya kwanza Kocha Mkuu mpya wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael, alionekana kufurahia namna wachezaji wa timu hiyo walivyokuwa wakimiliki mpira katika kipindi cha kwanza dhidi ya Mtibwa Sugar.

Eymael aliyetua nchini juzi na kuunganisha moja kwa moja visiwani hapa kutambulishwa kwa wachezaji, anarithi mikoba ya Mkongomani Mwinyi Zahera aliyetimuliwa hivi karibuni.

Katika mechi hiyo ya nusu fainali ya Kombe la Mapinduzi iliyopigwa juzi usiku, Nipashe lilikuwa likimfuatilia Eymael jukwaani akiwa na wenyeji wake viongozi wa Yanga na mara kadhaa alionyesha kufurahi pindi timu hiyo ilipomiliki mpira na kuonana kwa pasi.

Yanga ilionyesha mchezo mzuri kwa kucheza pasi za haraka haraka tofauti na mchezo uliopita dhidi ya Jamhuri ambao walishinda 2-0, na dakika ya 36 ilipata bao la kuongoza kupitia kwa Deus Kaseke.

Kuingia kwa bao hilo kuliongeza kujiamini kwa wachezaji wa Yanga na kuonyesha soka la kuvutia zaidi ambalo mara kadhaa lilimfanya Mbelgiji huyo kutabasamu.

Bao hilo lilidumu hadi dakika ya 90 kufuatia Shomari Kibwana kuisawazishia Mtibwa Sugar na hatimaye mikwaju ya penalti kuchukua hatua yake na Yanga kutolewa katika michuano hiyo kwa kufungwa matuta 4-2.

Kutolewa kwa Yanga kulizua 'vilio' na huzuni kubwa kwa baadhi ya mashabiki wa timu hiyo ambao walikuwa wakitamani itinge fainali sambamba na Simba ili washuhudie 'dabi' ya watani hao wa jadi.

"Tumeikosa dabi ya watani, hii Yanga imetupunguzia utamu wa Mapinduzi, wangepita na Simba kesho (jana usiku), tungeburudika sana," alisema shabiki mmoja aliyejitambulisha kwa jina la Maulid Abdullah.

Aidha, mjumbe mmoja wa Kamati ya Mashindano ya Kombe la Mapinduzi, ambaye aliomba hifadhi ya jina lake, aliliambia Nipashe kuwa kama ingetokea miamba hiyo kukutana ingeongeza mapato pia.

Kocha msaidizi wa Yanga, Said Maulid 'SMG' akizungumzia mchezo huo, alisema walijitahidi kupambana hadi mwisho lakini penalti hazina mwenyewe.

"Wapo wanaosema tumefanya makusudi ili kuikwepa Simba, hiyo si kweli kila mtu ameona namna tulivyopambana na kufika hatua ya penalti ambazo hazina mwenyewe," alisema mchezaji huyo wa zamani wa Yanga na Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Katika mechi hiyo ya juzi, Kipa wa Yanga, Ramadhani Kabwili alipangua penalti ya kiungo Abdulhalim Humud, hata hivyo, beki Kelvin Yondani aligongesha mlingoti na kiungo Abdul-Aziz Makame akapaisha juu ya lango.

Wafungaji wa penalti za Mtibwa Sugar walikuwa ni Omary Sultan, Dickson Job, Jaffary Kibaya na Shomari Kibwana na za Yanga zilifungwa na Paul Godfrey 'Boxer' na kiungo Mapinduzi Balama.

## Mambo magumu Simba, Yanga FA

**Na Somoe Ng'itu**

SAFARI ya kuwania tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika inatarajia kuendelea kwa Simba kupangwa kukutana na 'wababe' wao Mwadui FC wakati Yanga itawakaribisha Tanzania Prisons, imefahamika.

Mwadui ndio timu pekee iliyoifunga Simba katika mechi za Ligi Kuu msimu huu wakati Yanga ilipata ushindi mwembamba dhidi ya Tanzania Prisons walipokutana kwenye ligi hiyo hivi karibuni.

Mechi hizo za raundi ya nne ya mashindano hayo yaliyoanza kwa kushirikisha jumla ya timu 64 (Ligi Kuu, Ligi Daraja la Kwanza na Ligi Daraja la Pili), zitachezwa kati ya Januari 24 na 26, mwaka huu.

Pia katika droo hiyo iliyochezeshwa jana jijini Dar es Salaam, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), lilitangaza rasmi mchezo wa fainali ya mashindano hayo utachezwa Mei 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mkoani Rukwa.

"Hili litakuwa tukio la mwisho la kufunga msimu, fainali zitachezwa Mei 30, mwaka huu katika mji wa Sumbawanga, Rukwa, tunaipongeza mikoa yote iliyoingia katika mchujo wa kusaka mwenyeji," alisema Mkurugenzi wa Mashindano wa TFF, Salum Madadi.

Mabingwa watetezi Azam FC wao watavaana na timu ya Daraja la Kwanza, Friends Rangers ya Magomeni jijini wakati Gwambina itacheza dhidi ya Ruvu Shooting, African Sports wataikaribisha Alliance, Polisi Tanzania dhidi ya Mbeya City, Ndanda FC watawakabili Dodoma FC huku Majimaji FC ikiwa mwenyeji wa Stand United ya Shinyanga.

Ihefu FC ya Mbeya itacheza dhidi ya Gipco FC, wakongwe Pan Africans watawafuata KMC FC, Panama FC itacheza dhidi ya Mtwivila FC, Namungo FC itachuana na Biashara United, Mtibwa Sugar wao watawaita Sahare All Stars, JKT Tanzania na Tukuyu Stars, Kagera Sugar na Might Elephant huku Lipuli FC itachuana na Kitayosa.

Endapo Simba itasonga mbele itakutana na mshindi kati ya Majimaji na Stand United wakati Yanga itamsubiri mshindi kati ya Gwambina dhidi ya Ruvu Shooting na Azam FC itasafiri kumfuata mshindi kati ya Ihefu na Gipco.

Azam FC ilitwaa ubingwa huo baada ya kuwafunga Lipuli FC mabao 1-0 katika fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Ilulu, Lindi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >